# Kristo Amefunuliwa Katika Neno Lake Mwenyewe

Jeffersonville, Indiana USA

Agosti 22, 1965A

1 Na tuinamishe vichwa vyetu. Bwana Yesu, Mchungaji wa lile Kundi kuu, tuna deni sana na Wewe, Bwana, hata tusingeweza kukulipa kwa ajili ya upendo ambao umemwaga moyoni mwetu. Tunajisikia hatustahili sana tunapoinamisha vichwa vyetu na kusimama katika uwepo Wako. Tunakuomba utusafishe na makosa yote na dhambi zote. Tunaomba ya kwamba utaimarisha miili yetu leo. Wengi ni wagonjwa na wanaoteseka, kama inavyoonyesha hapa, kwa leso na maombi yanayokuja kwenye simu na kila mahali.

Nasi tunaamini ya kwamba tunaimalizia historia ya ulimwengu huu sasa, na hivi karibuni wakati utafifia katika Umilele, nasi tunataka kuwa tayari kwa ajili ya saa hiyo. Hiyo ndiyo sababu tumekusanyika hapa asubuhi ya leo, ni kujiandaa kwa ajili ya wakati huo. Nami nimeambiwa ya kwamba kuna wengi wanaosikiliza kwa simu asubuhi hii kila mahali nchini, kutoka pwani hadi pwani. Popote sauti zetu zinapokuja, jalia kundi hilo dogo libarikiwe. Waponye wagonjwa walio miongoni mwao, nami naomba ya kwamba utasafisha nafsi zao na maovu yote. Na utusaidie hapa asubuhi ya leo, maskanini, ili kwamba sisi pia tupate kufurahia majaliwa hayo makuu.

2 Nasi tunaomba ya kwamba utanena nasi leo kupitia kwa Neno Lako lililoandikwa, na jalia Roho atufunulie mambo tunayohitaji, kwa kuwa tumekusanyika nchi nzima sasa, tukijisikia ya kwamba sisi ni watu wadogo, bali tuna nafasi miongoni mwa waliokombolewa, kwa sababu tumemwamini Yesu Kristo. Tujalie mambo haya, Bwana.

Na wakati tunapofunga ibada na kwenda kwenye nyumba zetu mbalimbali nchini kote, na tuseme, kama wale kutoka Emau, "Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu alipokuwa akisema nasi njiani?"

Sasa, Baba, ninajua ya kwamba lo lote ningalisema bila shaka lingekuwa halitoshi, pamoja na—na Wakristo wazuri kote nchini sasa ambao wanasikiliza, lisingekuwa—lisingetosha. Isingekuwa ni kitu ambacho ningesema ambacho kingeweza kufaa kitu, kwa sababu sisi sote tuko katika kundi sawa. Sisi ni wanadamu, wenye kupatikana na mauti. Lakini hebu na Roho Mtakatifu mkuu anene; hebu alishike Neno na kujifunua Mwenyewe. Tunamngojea sasa, katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi.

3 Kwa namna fulani mimi … najishangaa mwenyewe. Nilimwambia mke wangu, kama ikitokea anasikiliza, huko Tucson, kwamba sikufikiri ningekuwa na ibada yo yote nitakaporudi; na hata sikuleta nguo. Nami nikamwambia mkwe wangu, alikuwa amepiga pasi koti langu, nami nikasema, "Ninakaa nyuma ya mimbara, kwa … Hawajui suruali ni aina moja na koti ni aina nyingine." Ni zile nilizovaa nyumbani. Bali, Meda, alipiga pasi shati langu na kila kitu, kwa hiyo kila… Usijali; kila kitu ni sawa.

4 Sasa, tuna ombi hapa, ya kwamba kuna ndugu mpendwa sana … Nami nafikiri ya kwamba—ya kwamba Prescott, naamini, wanasikiliza kwa simu asubuhi ya leo, kule—kule Prescott, Arizona. Baba yake Dada Mercier ndiyo kwanza awe njiani akija huku mkutanoni, ninavyofahamu, naye ilibidi apelekwe hospitali kwa ajili ya ugonjwa wa moyo, Ndugu Coggins. Na, pia, Ndugu Junior Jackson, nafikiri yuko kwenye redio inayofuata, ama simu inayofuata huko Clarksville ama New Albany, na baba yake yuko hospitalini, nafahamu, na upasuaji mkubwa wa kansa kwenye ini. Kwa hiyo tunataka hakika kuwakumbuka hao katika maombi yetu. Na sasa kuna wengine hapa, pia, bali hatutaki kuchukua wakati. Mungu anajua yote juu yao, kwa hiyo hebu na tuwaombee sasa.

5 Mungu mpendwa, kama vile yule mzee mpendwa mwenye mkono wenye makunyanzi, Ndugu Coggins, shujaa wa siku nyingi kwenye huduma, amekuwa…akiwa amelala hospitalini asubuhi ya leo, mahali fulani, akiugua ugonjwa wa moyo. Mungu, maskini moyo huo wa kale umepitia katika shida nyingi. Ninaomba, Mungu, umsaidia. Jalia hio. Yeye anapenda … Yeye anapenda maisha kama sisi sote tunavyopenda, naye anataka kuishi. Bwana Mungu, tujalie. Sisi kote nchini tunamwombea katika Jina la Yesu, ya kwamba utamponya na kumtoa. Tunaamini ya kwamba Wewe utafanya hivyo; atakuja moja kwa moja mkutanoni.

6 Tunamwombea Ndugu Jackson, baba yake wa thamani amelala pale karibu kufa sasa, naye alimleta ulimwenguni mvulana mzuri kama Junior. Na—na—naomba, Mungu mpendwa, ya kwamba utamponya. Ninajua inaonekana haiwezekani. Madaktari, madaktari, wao—wao hawajui la kufanya katika hali kama hiyo. Lakini tunamkumbuka Ndugu Hall, pia, wakati madaktari bora sana hapa walisema, huko Louisville, waliposema, "Ana masaa machache tu ya kuishi," akiwa na kansa kwenye ini. Naye anaishi leo, na hiyo ni miaka ishirini na mitano iliyopita, kwa sababu ya neema Yako. Kwa hiyo ninaomba ya kwamba utamponya Ndugu Jackson leo, Bwana, jalia neema Yako na rehema ziwe pamoja naye.

Na lundo hili lote kubwa la leso na vitambaa na kadhalika ambavyo vimewekwa hapa katika maombi; Unawajua wote, Baba. Ninaomba ya kwamba utawapa uponyaji wote hao. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

7 Sasa anza, asubuhi ya leo, sikufikiri ya kwamba ningeshuka, kwanza, Jumapili iliyopita. Na halafu tena, tulipolitangaza jambo hilo, nilishuka nikaja. Ndugu Neville alinifanya nizungumze! Na kisha

tukatangaza kuwa huko chini leo, na haijatangazwa kwa watu kote nchini. Nasi tuna mfumo huu wa simu sasa, ambao ni mzuri sana. Watu wanaweza kuketi moja kwa moja majumbani mwao ama wao … kukusanyika mahali pao, makanisani mwao, na kadhalika, na kusikia ibada. Ninathamini jambo hilo.

8 Sasa ninaona yamewekwa hapa, kulikuwa na maombi mengi juma hili lililopita, juu ya yale niliyosema Jumapili iliyopita juu ya Ujumbe. Ninaamini ninasahau kile nilichokipa jina sasa. Lakini nilisema jambo fulani kuhusu kulipa madeni yenu. Na unajua, haidhuru unasema nini, linaeleweka vibaya na watu. Si kwa sababu wao wana-…wao hawataki kulielewa vibaya, bali unalielewa vibaya tu.

Na sasa mtu fulani alisema, "Je! Tununue gari?" Ama, "Nifanye nini …"

Sasa, hilo silo Yesu alilosema, ama Biblia pale, lililosema, "Msiwiwe na mtu cho chote." Hayo ni madeni ya muda mrefu ambayo ungeweza kulipa. Walipeni. Si … Huko ni kutowiwa na mtu cho chote. Haimaanishi … Jamani, tunadaiwa kodi yetu, bili yetu ya simu, sisi … na kadhalika. Tu—tunadaiwa mambo hayo, na tunayalipa. Lakini, deni la zamani ambalo ungeweza kulipa, lilipe. Mnaona? Sasa, usiende na kitu chochote kinachoning'inia namna hiyo.

9 Ninakumbuka wakati nilipokuwa mgonjwa, wakati mmoja nilipokuwa mvulana. Nilitoka hospitalini nikidaiwa kama dola elfu mbili. Na kulikuwa na duka la madawa hapa, Bw. Swaniger, aliniwia kama dola mia tatu ama mia nne, bili ya madawa. Hata hakunijua. Na mtu huyo … Nilimwendea. Sikumjua. Naye aliituma tu kule, hata hivyo, hakukataa kuituma.

Nami nikasema, "Uninawia." Nami nikasema … Ninaamini, Swaniger … Nami nikasema… Naamini, Swaniger…Ilikuwa Bw. Mason kule chini kwenye Barabara ya Court na Spring. Nami nikasema, "Uninawia. Nami—nami bado ni dhaifu sana, bali ninajaribu kwenda kazini. Sasa, kama siwezi kuwalipa …" Nilikuwa tu ndiyo kwanza niwe Mkristo. Nikasema, "Jambo la kwanza, Bw. Mason, kama jukumu langu kwa Mungu, Yeye ananiwia zaka zangu. Ninataka kumlipa fungu langu la kumi, kwanza." Nami nikasema, "Basi wajibu wangu unaofuata ni kulipa madeni yangu." Nikasema, "Baba yangu ni mgonjwa, na yeye … Nasi tuna … Tuko watoto kumi katika familia." Lakini nilisema, "Nita … Kama siwezi kuwalipa zaidi ya senti ishirini na tano kwenye bili hiyo, kila siku ya malipo; kama siwezi kukulipa hata senti ishirini na tano, nitakuja na kukwambia kuhusu hilo. Nitakwaambia, 'Si—si—siwezi kufanya hivyo wakati huu.'" Sasa, kwa msaada wa Mungu, nililipa kila senti yake. Mnaona? Lakini hilo ndilo ninalomaanisha, mnaona? Mtu asiseme tu …

10 Loo, Mkristo fulani hapa kanisani wakati mmoja aliondoka akaenda akatengenezewa motokaa hapa, naye mtu huyo akamjia… Mtu huyo akasema, "Nitakulipa. Huwa ninalipwa Jumamosi," ama kitu kama hicho. Wala hakumlipa kamwe. Na majuma baada ya majuma yalipita, na kamwe hakumlipa, hata hakusema neno kamwe. Na—na mtu huyo akaja na kuniuliza, akasema … Mnaona, inaakisi kinyume cha kanisa. Inaakisi kinyume cha Kristo.

Huwezi kumlipa, nenda ukamwambie, useme, "Nina deni lako, nami nitakulipa. Mimi ni Mkristo, bali ni—ninaninii tu … Siwezi kufanya hivyo sasa hivi, nina … Ninawiwa hili." Na, kumbukeni, iko kwenye vitabu vya Mungu pia, mwajua, kwamba mnawiwa. Kwa hiyo hilo ni … Ninajaribu, kwa ajili yangu mwenyewe na kwa ajili yetu sisi sote pamoja, kujaribu kuwa tayari, kwa kuwa tunajua tunakaribia jambo fulani, karibu sana na jambo fulani litakalotukia. Kwa hiyo tunataka kuwa tayari. Wakati kule Kuja kwa Bwana kunapokaribia sana sasa, tunataka kuwa tayari kwa ajili ya ile saa kuu.

11 Sasa tunataka kuwa tayari na kuzungumza sasa juu ya somo dogo hapa ambalo nililichagua asubuhi ya leo, kwa msaada wa Bwana. Nasi tutazungumza kwa kifupi tu tuwezavyo, kwa sababu ya mawasiliano ya simu na watu. Natumaini ninyi nyote mna ninii … kote nchini, mna asubuhi nzuri kama tuliyo nayo hapa Indiana. Hali ya hewa nzuri, ya baridi, nzuri tunayo sasa tangu mvua iiliponyesha. Na ni nzuri sana.

12 Sasa nataka kusoma kutoka katika Kitabu cha Waebrania, mlango wa 1; na kutoka kwenye Kitabu cha Yohana Mtakatifu, sura ya kwanza kabisa. Waebrania 1:1 hadi 3, na Yohana Mtakatifu 1:1, kwa ajili ya somo. Somo langu asubuhi ya leo ni somo katika Maandiko. Sasa hebu na tusome Waebrania 1:1.

> *Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi;*
>
> *Lakini mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu;*
>
> *Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na ... chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu; Ni usomaji mzuri jinsi gani! Sasa Yohana Mtakatifu 1:1.*
>
> *Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*

13 Sasa, na somo langu asubuhi ya leo ni: *Kristo Amefunuliwa Katika Neno Lake Mwenyewe*. Sasa,

mahali nilipofikia mwisho wa kuzungumza juu ya jambo hili, ilikuwa ni kwa sababu … Tukijua ya kwamba yale tusemayo hatupaswi kuyasema tu kwa sababu tumekusanyika pamoja kuzungumza tu juu ya jambo lo lote kwa kubahatisha, bali ni jambo litakalosaidia kuwatuliza watu, kwa kuwa tutapita kwenye maji hatari, ya udanganyifu. Tayari tunapitia kwenye hayo. Na wakati mwingine nafikiri kwenu ni kama ilivyo kwangu, ya kwamba inaonekana hivyo, mengi sana, yanatisha sana.

14 Nilikuwa tu nikizungumza na mhudumu kijana na mkewe, chumbani, dakika chache tu zilizopita. Na wote wawili wana wasiwasi kama tu ulimwengu mwingine wote, wanadamu wengine duniani. Nikasema, "Kumbuka, Shetani anakupiga ngumi." Sijali wewe ni nani, Mungu … Yeye ana haki ya ngumi hiyo moja. Ungalitaka upate nini, upate hiyo ngumi; uwe kipofu, ama uugue yabisi kavu ukiketi kwenye kiti cha kusukumia wagonjwa, ama uwe na wasiwasi? Mnaona? Yeye ana mahali fulani ambapo anaweza kukupiga ngumi. Yeye ana haki ya mahali hapo pa wazi. Sasa, hapo ndipo mahali unapopaswa kuendelea kufunikwa wakati wote. Na kuona wakati huu wa wasiwasi tunaoishi!

15 Na kanda za juma lililopita, nafikiri, zitawafunulia mambo makuu sana ya kuchukiza ambayo tutazungumza habari zake moja ya siku hizi wakati tutakapoweza kupata nafasi ya kutosha, juu ya kufunguliwa kwa yale mapigo ya mwisho yatakayomwagwa juu ya nchi , vile Vitasa, hasa, kumiminwa kwa vile Vitasa, na zile Ngurumo Saba, na mambo hayo ya kutisha yanayokuja duniani. Mwanadamu sasa, na watu siku hizi, wako katika hali ya fadhaa sana; ulimwengu mzima!

16 Ukisoma Reader's Digest ya mwezi uliopita, utaona somo hapo; ni kwa Billy Graham, yule mwinjilisti mashuhuri. Alichoka sana hata hakuweza kufanya mikutano yake, naye—naye akaenda kwenye zahanati ya Mayo kwa uchunguzi wa mwili. Hakukuwa na kosa lolote kwake, ila tu yeye hafanyi kazi ya kutosha. Nao wakamfanya awe anakimbia; mazoezi ya mwili. Yeye huendesha maili moja kila siku.

Na ndipo makala hayo yanaendelea kusema ya kwamba sayansi imethibitisha ya kwamba leo hii, ya kwamba watoto wadogo, hawa wavulana na wasichana, "wanafikia umri wa utu uzima kwenye umri wa miaka ishirini." Na ifikapo ishirini na mitano, mara nyingi, katika visa vingi, wasichana wameisha kukoma hedhi, wakiwa na umri wa miaka ishirini na mitano.

Sijui kama ulijua jambo hilo ama hujui, lakini siku chache zilizopita usiku wakati Roho Mtakatifu alipokuwa akinena hapa mkutanoni, msichana mdogo ameketi hapa chini, hiyo ndiyo hasa ilikuwa shida ya mtoto huyo wakati ilipoita. Nikamwangalia mara ya pili, nikatazama tena, nami nikaona shida ilikuwa ni nini. Nikawaza, "Haiwezekani; mtoto huyo ni mdogo sana." Bali ilikuwa ni kuingia ugumba, yapata umri wa miaka ishirini, ishirini na mitatu, kitu kama hicho. Mnaona?

17 Mama yangu na mama yako walifikia umri huo yapata miaka arobaini na mitano hadi hamsini. Mke wangu alipita umri huo yapata miaka thelathini na mitano. Sasa imefikia ishirini. Jamii yote ya binadamu imeoza. Vema, kama hiyo miili ya utu wetu wa kawaida inararuka-raruka namna hiyo kutokana na kula vyakula vya kisasa, mahangaiko, ambayo yameiozesha, je! mambo hayo hayaozeshi chembechembe za ubongo? Ndipo tunaweza kuona jinsi wanawake wanavyoweza kuingia barabarani, uchi. Tunaweza kuona jinsi wanavyoweza kuendesha magari mbio ba—barabarani kwenye mwendo wa maili mia na ishirini kwa saa, mambo haya yote. Imefikia mahali ambapo taifa zima, ulimwengu mzima, si taifa hili tu, bali kila mahali, wamepotea kiakili.

18 Halafu basi tutakapofungua hayo, Bwana akipenda, kwenye vile Vitasa Saba na kuonyesha mambo hayo ya kuchukiza. Watu watakuwa wenda wazimu sana, baada ya kitambo kidogo, mpaka watawazia wanaona chungu wa ukubwa wa mlima. Itakuwa ikiwatesa wanawake; nzige waje duniani, wenye nywele ndefu, kuwatesa wanawake wanaokata zao; nywele kama wanawake, zikining'inia chini; na meno marefu, kama simba; miiba katika mkia wao, kama nge, na—na kadhalika, kuwatesa wanadamu juu ya nchi. Lakini basi itakuwa ni kuchelewa sana kufanya lolote juu yake. Iweni sawa sasa. Mnaona? Kuwatesa!

19 Na Jumapili iliyopita tulipokuwa tukipitia kwenye hiyo miviringo, jinsi ambavyo hizo hisi tano kwenye milki ya nje. Hiyo ndiyo njia ya kuingia, hisi tano za mwili. Kuna njia moja tu unayoweza kuingia katika huo mwili, hiyo ni kwa hizo hisi tano: kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Hakuna njia nyingine ya kuwasiliana na—na mwili.

Ndani ya mtu huyo kuna mtu anayeitwa roho, naye ana hisi tano: kuwaza, wazo…na mawazo, na upendo, na dhamiri, na kadhalika. Sawa kabisa.

Sasa, huwezi kuwaza kwa mwili wako. Unawaza kwa akili yako. Na hapo ndani ndipo ambapo wengi sana, wa Wakristo, wanasimama tu. Nao wanaweza, kama tu mahindi shambani na magugu shambani, wanaweza kutiwa mafuta na Roho Mtakatifu yule yule ambaye anamtia mafuta mwamini.

Lakini chini ndani ya hiyo, milki inayofuata, milki ya tatu, ni nafsi; na hilo limechaguliwa tangu asili na Mungu. Hapo ndipo inapokaa ile mbegu-hai iliyo halisi, iko mle ndani.

Na, kumbukeni, kama ningechukua gugu na kulipasua, nilipandikize kwenye moyo wa—wa ngano na kuliweka pale, nilifukie, litazaa ngano kutoka kwenye hilo gugu; haidhuru mle ndani mna nini, ni misisimko

gani.

20 Leo, tumechanganyikiwa sana kuhusu ushahidi wa Roho Mtakatifu, na kadhalika. Shetani anaweza kuiga karama ya aina yo yote aliyo nayo Mungu, bali hawezi kuleta hilo Neno, Neno kwa Neno. Hapo ndipo aliposhindwa katika bustani ya Edeni. Hapo ndipo yeye aliposhindwa. Hapo ndipo wao, ile kanda juu ya "watiwa mafuta, wa uongo," ama watiwa mafuta; wao wanaweza kutiwa mafuta na Roho, wanene kwa lugha, wacheze dansi, wapaze sauti, wahubiri Injili, na wangali ni Ibilisi.

Ni mle ndani! Sasa kumbukeni, Yesu alisema, "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu kwanza."

Sasa, tumepitia kwenye somo, kuonyesha ya kwamba katika … Ulikuwa katika babu wa babu wa babu wa babu, huko nyuma kabisa, ukinena kimwili. Halafu, hivyo ndivyo ulivyo katika mwili, maumbile. Wakati mwingine mtoto atazaliwa katika familia, mwenye nywele nyekundu. Inamshangaza baba, maana hakuna mtu anayemjua, wa watu wake, mwenye nywele nyekundu, ama wa mama. Lakini kama utarudi nyuma kwenye vizazi kadhaa, utaona mtu fulani alikuwa na nywele nyekundu. Mbegu hiyo inaendelea kushuka chini, nawe unakuja asili ya mmoja kutoka huko nyuma kabisa.

Kama vile Waebrania sura ya 7 ilivyosema, ya kwamba, "Melkizedeki, Ibrahimu alimlipa fungu la kumi wakati alipokuwa akirudi kutoka kuwaua wafalme. Naye Lawi, aliyepokea sehemu ya kumi, alitoa sehemu ya kumi," kwa maana alikuwa katika viuno vya Melkizedeki kwenye … ama,"viuno vya Ibrahimu," hasa, wakati alipokutana na Melkizedeki.

21 Sasa jambo lile lile ni hili. Kama wewe ni mwana wa Mungu, na kama mimi ni mwana wa Mungu, ama binti wa Mungu, tulikuwa katika Mungu hapo mwanzo. Na wakati Yesu alipofanyika utimilifu wa Neno, basi tulikuwa ndani Yake, umbo la seli zazi. Wakati aliposulibishwa, tulisulibishwa katika mwili Wake. Alipofufuka katika wafu, tulifufuka pamoja Naye. Na sasa, kwa kuwa tumelitambua, "sasa tunaketi pamoja Naye, katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu." Mnaona? Kwa kuwa Yeye … Sisi, kama sisi ni wana na binti za Mungu, sisi ni watoto wa Mungu, basi sisi ni sifa za Mungu. Ndipo tulikuwa … tukapata Uzima wa Milele. Na Mungu ndiye Uzima wa Milele pekee uliopo. Ndipo, tulikuwa ndani Yake tangu mwanzo. Na wakati Yesu alipofanyika Neno hilo lote, basi tulikuwa sehemu Yake wakati huo. Amina! Haya basi. Hicho kitu kinapokuwa mle ndani, hamna ibilisi, hakuna mamlaka, wala hakuna kitu kinachoweza kukitikisa. Hicho ndicho knguzo ya kushikilia nafsi.

Unaweza kupakwa mafuta *hapa* nje, katika roho hii, na kutamani, na kufanya mambo haya mengine yote. Lakini inapofikia kwenye nguzo hii ya kushikilia Neno hilo, kamwe hutatoka hapo. Litashikilia moja kwa moja imara na kweli, kwa Neno hilo, kadri iwezavyo kuwa. Nje ya jambo hilo, haidhuru unafanya nini, ungali umepotea.

22 Wakati huo wa Kanisa la Laodikia, "uchi, kipofu, wenye mashaka; Hata hawajui." Mnaona, ni nje … Ni yule aliyetiwa mafuta, aliyetiwa mafuta na Roho halisi. Mnaona, ya kwamba Roho Mtakatifu anaweza kushuka juu ya mtu, katika roho yake. Lakini nafsi yake ni chembechembe yake hai; hiyo chembechembe hai ni Neno. Mnaona? Na namna … Sijali unaweza kuhubiri kiasi gani, namna unavyofanya jambo *hili* vizuri, na jinsi unavyopenda; huo ni mmojawapo wa milango ya roho. Huwezi kupenda kwa mwili wako; unapenda kwa roho yako. Hiyo ni moja ya milango. Nawe unaweza kumpenda, na hata kumpenda Mungu, na bado usiwe sahihi. Unaweza kutoa pepo, na kuhubiri, na kufanya mambo haya; bado si sawa. Yesu alisema hivyo, alisema wengi wangekuja siku hiyo. Neno hilo linatosha!

> *Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*
>
> *Naye Neno akafanyika mwili, akakaa kwetu, …*

23 Angalia, nitazungumza juu ya somo hili la Biblia, la, *Kristo Akifunuliwa Katika Neno Lake Mwenyewe.* Mahali nilipofanya maamuzi haya, ilikuwa chumbani mwangu.

Mtu fulani mpendwa, huenda ameketi hapa asubuhi ya leo … Nina picha inayoning'inia kwenye chumba changu cha kujisomea kule juu, hiyo ni picha iliyochorwa na Hofmann ya Kichwa cha Kristo, imeandikwa katika zile Sifa za Heri. Na hapo unapofikia mahali ambapo ungehitaji sehemu ya nywele, wanakandamiza kidogo zaidi kwa kalamu unapopitia sehemu hiyo. Hapo, huyo hapo, ameketi katika Neno Lake, akiangalia moja kwa moja; Kristo katika Sifa za Heri. Mtu fulani, ye yote yule, ninakushukuru kwa ajili ya jambo hilo.

Na mtu fulani akaileta picha hiyo na kuiweka kwenye chumba changu cha kusoma pale, ya Eliya akipanda juu katika gari la moto. Tunathamini mambo haya. Mara nyingi, makundi makubwa, sipati tu nafasi ya kunena na kusema mambo haya, bali ninayaona, ndugu, dada. Ni—ninajua jambo hilo, na Mungu analijua.

Sasa nitazungumza juu ya somo hili la: *Kristo Akifunuliwa Katika Neno Lake Mwenyewe.* Jinsi

ambavyo, katika zile Sifa Heri, kuna picha ya Kristo, amesimama moja kwa moja, kama. Hapo ndipo nilipowazia juu ya somo hili. Sasa, Kristo na Neno ni kitu kimoja. Mnaona?

24 Wanasema, "Biblia ilikuwaje …?" Watu wanasema. Nilikuwa nikiendesha gari na mtu fulani si muda mrefu uliopita. Akasema, "Wazia jambo hilo. Sisi hapa duniani, namna tulivyo, na tunajua tu ama tunaweza kusema tu kwamba tumeokolewa na hadithi fulani ya Kiyahudi inayoitwa Biblia."

Nikasema, "Bwana, sijui jinsi unavyosema jambo hilo, bali siamini ni hadithi ya Kiyahudi," nikasema.

Akasema, "Vema, unaomba, unaomba kwa kitu gani? Niliomba kitu fulani na mambo fulani; Sikukipata."

25 Nikasema, "Unaomba vibaya. Hatupaswi kamwe kuomba kubadilisha nia ya Mungu; tunapaswa kuomba kubadilisha nia yetu. Nia ya Mungu hahitaji kubadilika kwo kwote. Mnaona? Mnaona, ni kweli." Nikasema, "Siyo kile ulichoomba …"

Ninamjua mvulana mmoja Mkatoliki, wakati mmoja, alikuwa na kitabu cha sala, akikariri sala, na kwa kusudi mama yake apate kuishi. Naye akafa, naye akakitupa kitabu cha maombi motoni. Vema, mnaona, sikubaliani na kitabu cha sala; lakini, hata hivyo, mnaona, unachukua mtazamo mbaya. Unajaribu kumwambia Mungu la kufanya.

Maombi yanapaswa kuwa, "Bwana, nibadilishe nilingane na Neno Lako." Si ati, "Badilika," si, "hebu naomba nibadilishe nia Yako. Unabadilisha nia yangu." Mnaona? "Unabadilisha nia yangu iwe mapenzi Yako. Na mapenzi Yako yameandikwa hapa katika Kitabu. Na, Bwana, u—usiniache niondoke mpaka umeifanya nia ya—nia yangu kuwa kama nia Yako. Na kisha nia yangu itakapokuwa kama nia Yako, ndipo nitaamini kila Neno uliloandika. Nawe ulisema, mle ndani, utafanya kila kitu 'kitende kazi kwa manufaa' kwa wao wakupendao Wewe. Nami nakupenda, Bwana. Yote ni kufanya kazi pamoja kwa manufaa."

26 Nimekuwa hapa nchini juma hili, nikikaa na marafiki wapendwa sana. Niliwauliza baadhi yao mezani, jana, tulipokuwa tukila. Daima tunaketi hapa na kufanya ninii ndogo … kama kusoma kidogo juu ya Biblia. Nilikuwa nikizungumza juu ya upendo.

Na kulikuwa na mtu fulani aliyeniambia, akasema, "Ninaamini wewe ni mpinga-Kristo."

Nikasema, "Kama hilo lingempendeza Bwana wangu, hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa. Ninataka kuwa chochote anachotaka niwe. Ninampenda. Na kama akinitupa kuzimu, bado nitampenda, kama nikienda na roho yule yule niliye naye sasa." Aliniangalia kwa namna ya ajabu.

Niliwaona wanne ama watano wao pale, wanaume vijana; wake za watu vijana, wanawake wazuri. Nilijua jinsi hao wavulana walivyowapenda wake zao, kwa hiyo nikawaambia, nikasema, "Hii hapa njia ya kulijaribu. Kama mke wako, kabla hujafunga ndoa … Sasa, rudi nyuma, tuseme wewe… maisha haya ya ndoa, umekuwa ukiota ya kwamba umeoa; kwa kweli hukuwa umeoa, bali uliota ulikuwa umeoa. Nawe ukaamka, ukaenda na kuzungumza jambo hilo na mpenzi wako, na kusema, 'Unajua, niliota ya kwamba tulikuwa tumeoana, na tulikuwa na watoto. Sisi tunaishi kwa furaha, na—na tunakungojea Kuja kwa Bwana, na kila kitu.' Na halafu msichana huyu angekuambia, 'Unajua, nampenda mwanamume mwingine kuliko ninavyokupenda. Ningeweza kuwa mwenye furaha zaidi pamoja na huyo mwanaume mwingine.' Je, ungeweza, kutoka moyoni mwako, kumpenda vizuri vya kutosha kusema, 'Baraka za Mungu na ziwe juu yako, mpenzi wangu. Nenda na mtu huyu mwingine?"

Sasa, sasa angalieni jambo hilo, kila mmoja wenu wanaume au ninyi wanawake. Mnaona? Vema, kama upendo wenu ni sahihi, mngefanya hivyo, kwa kuwa unajali mafaniko yake. Vipi, unajua ungeweza kumpata, unaweza kumwishia, wewe… Ni mke wako; atakuwa mkeo. Utamwoa, bali hatakuwa na furaha. Angekuwa na furaha zaidi … Halafu basi, kama unampenda, basi unataka yeye awe na furaha.

Kwa hiyo, chochote mapenzi ya Mungu yalicho, acha mapenzi ya Mungu yatendeke, kama ninafurahia jambo hilo au la. Ninataka kuishi kusudi Yeye apendezwe na yale ninayofanya. Kwa hiyo angalia ninii—kusudi lako na nia yako kwa jambo hilo; unajua kama unampenda Mungu au la.

Vipi kama Yeye angesema, "Utanitumikia kama nitakutupa?"

"Ninakupenda, hata hivyo."

27 Kwa hiyo, kama makanisa yangeona jambo hilo na yangeweza kuamini kwa namna hiyo, isingekuwa mmoja kujaribu kumnyang'anya jamaa mwingine mpira wakati anakimbia nao. Angekuwa anamlinda huyo. Mnaona? Wakati, nia halisi na kusudi halisi, hakungekuwa na mtu anayejaribu kusema, "Jamani, nina hili pia! Ni mimi, *huyu* ni mimi, *huyu*." Mnaona, Mungu hawezi kumtumia mtu. Kuna uigaji mwingi sana unaofuata, na huyo ni Shetani. Nao watu hawawezi kutambua jambo hilo. Wanajaribu kuuchukua mpira kutoka kwa mtu fulani aliyepewa. Hebu Mungu na ainue huduma fulani na angalia ni wangapi wanaoifuata. Mnaona? Mnaona?

28 Sasa, upendo halisi kwa Mungu, "Haidhuru mimi ni sehemu gani, Bwana, kama ninaweza tu kusema neno kwa ajili Yake, nisaidie kuulinda, hebu nifanye hivyo." Mnaona?

Hilo ndilo jambo lile lile lingekuwa kuhusu mke wako. Kama kweli unampenda, mnaona, si—si upendo wa—wa phileo; ni upendo wa Agape, upendo halisi. Yeye angeishi na mtu mwingine, akiwa na furaha zaidi; sasa bado wewe hujamuoa, bila shaka, huwezi.

29 Na, hebu kidogo, watu wanaosikiliza kanda hizi. Wengine, wengi sana, hutuma barua, wanasema, "Mbona, katika Ndoa Na Talaka, ulisema hivi na ulisema vile." Nilisema jambo hilo mara nyingi sana; kanda hizi huenda tu … Ninazungumza na kusanyiko langu, ndugu. Mimi siwajibiki na wale Mungu aliokupa kuwachunga; mimi ninawajibika na aina ya Chakula ninachowalisha watu hawa. Hii ni kwa ajili ya maskani hii pekee. Mnaona? Sasa, kama watu wanataka kusikiliza kanda, hiyo ni juu yao. Lakini ninazungumza na wale Mungu alionipa. Dhambi zao ndizo zilizoondolewa.

Mtu fulani aliandika, na kusema, "Vema, nilifanya *hili* na nilifanya *lile*. Ulisema dhambi yetu …" Si—sikusema jambo hilo.

Nikasema, "Angalieni jambo hili; hii ni kwa ajili ya watu hawa papa hapa, watu walio hapa maskanini, kundi langu mwenyewe." Sasa, kama watu wanataka kutengeneza chakula cha kisasa na kadhalika huko nje, wewe—wewe pata ufunuo kutoka kwa Mungu kisha ufanye yale ambayo Mungu anakwambia ufanye. Nitafanya jambo lile lile. Lakini Jumbe hizi ni za kanisa hili.

30 Angalia sasa, tunarudi, hatuna budi kuwa na kitu kingine ambacho hatuna budi kushikilia. Kitu fulani hakina budi kuwa nguzo ya kushikilia, kwa maneno mengine, ni mkataa. Na kila mtu hana budi kuwa na mkataa ama yakini. Nilihubiri juu ya jambo hilo wakati mmoja, miaka mingi iliyopita, kuhusu yakini, mahali ambapo ni neno la mwisho.

Kama vile mwamuzi kwenye mchezo wa mpira, kama anasema ni goli, hivyo ndivyo ilivyo hasa. Haidhuru umelionaje, mwamuzi alisema ni goli. Ulisema, "Mi—Mi—MiMI … Halikuwa goli. Lilienda … Niliona ninii …" Haidhuru ni nini, wakati aliposema, "goli," hivyo ndivyo ilivyo, hilo latosha tu. Yeye, yeye ndiye mkataa.

Na taa ya barabarani ni mkataa, kama inasema, "nenda." Unasema, "Vema, mimi, nina haraka, nina …" La, la. Inasema, "Wewe simama kimya wakati jamaa huyo mwingine anapoondoka." Mnaona? Ni mkataa.

31 Sasa, hapana budi kuwe na mkataa kwa kila kitu ufanyacho. Ilibidi kuwe na mkataa wakati ulipomchagua mke wako. Ilibidi kuwe na mwanamke uliyemchagua.

Sasa, hapana budi kuwe na wakati ambapo, wakati utakaponunua gari, utafanya mkataa wa aina gani. Je, itakuwa Ford, Chevy, Plymouth, gari la kigeni, chochote kile, huna budi kuwa na mkataa.

Na ndivyo ilivyo na maisha ya Kikristo. Hapana budi kuwe na mkataa.

32 Sasa, kama mtu fulani alisema, alimwendea mtu mwingine na kusema … alimsikia mtu fulani akisema, "Vema, unapaswa kubatizwa," na jamaa huyu kamwe … Labda, ninii yake, kanisa fulani ambalo halikubatiza, walinyunyizia tu. Nafikiri, tuseme kwa mfano, Wamethodisti, wao hubatiza kama mtu akiombwa, nasikia. Au labda ninii … Mkatoliki, nafikiri wananyunyiza tu. Kwa hiyo basi kama—kama mtu alisikia jambo fulani kuhusu "kuzamishwa majini," vema, yeye hakuelewa hilo; alilelewa Mkatoliki. Kwa hiyo anaenda kwa kuhani, na kusema, "Baba, nafahamu ya kwamba tunapaswa kubatizwa kwa kuzamishwa. Kanisa letu linasema nini kuhusu jambo hilo?"

"Mbona, inasema ya kwamba—ya kwamba inatupasa kunyunyiziwa." Kama kanisa hilo ndilo mkataa wake, hilo latosha. Mabishano yote yamekwisha; kanisa lilisema hivyo, na hakuna lingine.

33 Vipi kama ninii … kama ndugu Mbatisti alitusikia tukisema ya kwamba tunaamini katika kubatizwa kwa "kuzamishwa"? Angesema, "Ninaamini hilo."

"Na katika Jina la 'Yesu Kristo.'"

Sasa, huyu—huyu mfuasi wa kanisa anarudi kwa mchungaji na kusema, "Mchungaji, nilimsikia jamaa fulani akiniambia ya kwamba inatupasa kubatizwa kwa kuzamishwa, sawa, bali katika Jina la 'Yesu Kristo.'"

"Vema," yeye angesema, "sasa, hebu tuone. Mbona, hapa kitabu kinasema ya kwamba tunapaswa kubatizwa kwa kutumia 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.'" Kama kanisa hilo ndilo mkataa, hilo linatosha. Yeye hajali vile kitu kingine chochote kinavyosema; huo ndio mkataa wake.

34 Vema, kila dhehebu ni mmataa kwa waamini wao.

Lakini, kwangu mimi, na kwa wale ninaotumaini ya kwamba ninawaongoza kwa Kristo, na kwa Kristo, Biblia ndiyo mkataa wetu. Haidhuru … Maana, Mungu alisema, "Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu

liwe Kweli." Nami ninaamini ya kwamba Biblia ni mkataa wa Mungu. Haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini; Ni mkataa.

Biblia si kitabu cha mifumo. La, bwana. Si kitabu cha taratibu, wala kanuni za maadili.

Biblia si kitabu cha taratibu, taratibu nyingi sana, na kadhalika. La, bwana. Si kitabu cha maadili. La, bwana. Sivyo. Wala si kitabu cha historia, kabisa. Ama, wala si kitabu cha theolojia. Kwa kuwa, ni ufunuo wa Yesu Kristo.

Sasa kama mngetaka kusoma hayo, ninyi mlio na makaratasi yenu, mkiyaandika, huo ni Ufunuo 1:1 hadi 3, kama, Biblia ni "Ufunuo wa Yesu Kristo."

35 Hebu na tulisome tu wakati tuna wakati. Ninaamini ninii yangu … sina maandishi mengi sana hapa ya kuzungumza. Kama Bwana akikawia, mbona, tutajaribu kupata kutoka hizo.

> *Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi; naye akatuma kwa mkono wa malaika akamwonyesha mtumwa wake Yohana;*
>
> *Aliyelishuhudia Neno la Mungu, na ... ushuhuda wa Yesu Kristo, yaani, mambo yote aliyoyaona.*
>
> *Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu.*

36 Kwa hiyo, Biblia ni ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo. Nayo iliandikwa na manabii. Waebrania 1:1, katika … "Mungu, Ambaye alisema na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, katika siku hii ya mwisho ananena nasi kwa Mwanawe, Yesu Kristo," ambaye alikuwa manabii, wote, wakiwekwa pamoja. Yesu alikuwa Malaki; Yesu alikuwa Yeremia, Isaya, Eliya. Yote waliyokuwa, yalikuwa ndani Yake. Na yote uliyo, na yote niliyo mimi, yamo ndani Yake; Maneno, mashahidi wa Neno.

Kwa hiyo si kitabu cha taratibu, kanuni za maadili, wala si kitabu cha historia, wala kitabu cha theolojia. Sivyo. Lakini ni ufunuo wa Yesu Kristo, Mungu Mwenyewe aliyefunuliwa, kutoka Neno hadi mwili. Hivyo ndivyo ilivyo. Biblia ni Neno, na Mungu ni mwili, Mungu katika … Mungu ni Neno, hasa, na Yesu akiwa mwili. Ni ufunuo, jinsi Mungu (Neno) alivyodhihirishwa katika mwili wa mwanadamu, na kufunuliwa kwetu. Na hiyo ndiyo sababu Yeye anakuwa Mwana wa Mungu; Yeye ni sehemu ya Mungu. Mnaelewa? Sasa, Yeye si … Mwili ni sehemu ya Mungu, kiasi kwamba ni Mwana.

37 Mwana, kama vile Mkatoliki anavyosema, "Mwana wa Milele," na makanisa mengine yote; neno hilo hata halina maana. Mnaona? Hakuwezi kuwa na Milele, halafu kuwe na Mwana, maana Mwana ni kitu ambacho "kimezaliwa kutoka." Na neno Milele, Yeye hawezi kuwa Milele- … Yeye anaweza kuwa Mwana, bali hawezi kuwa Mwana wa Milele. La, bwana. Hakuwezi kuwa Mwana wa Milele.

Sasa, lakini Yeye ni Mwana, sana, hata Neno lote lililokuwa katika Yeremia, katika Musa, na Maneno hayo yote, kama vile Yeye alivyosema, "Wananena habari Zangu." Ufunuo huo wote wa kweli wa Kiungu wa Neno ulifungwa na kuwa mwili mmoja wa kibinadamu, na Mungu akaweka mwili kuuzunguka. Hiyo ndiyo sababu aliitwa "Mwana," sababu ya Yeye kutaja, "Baba." Mbona, ni rahisi tu, kama ukimwacha tu Mungu aimwage ndani ya moyo wako. Mnaona? Mungu alijifunua katika mwili wa nyama, angalia, kufunuliwa kutoka kwa mwili … au kutoka Neno kuingia mwili. Hiyo ni Yohana Mtakatifu 1:14, "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu."

38 Sasa angalia Biblia hii. Baadhi yao walisema, "Loo, vema, imefanya hivi, imefanya vile." Lakini hebu niwaambie jambo fulani, hebu tu …

Hebu na tuingie katika historia ya Biblia, kwa dakika moja tu, tuone mahali ilipotoka. Iliandikwa na waandishi arobaini mbalimbali. Watu arobaini waliandika Biblia, kwa muda wa miaka elfu moja mia sita, na katika nyakati mbalimbali, wakitabiri matukio muhimu sana yaliyowahi kutokea katika historia ya ulimwengu, na, mara nyingi, mamia ya miaka kabla haijatukia. Na hakuna hata kosa moja katika Vitabu vyote sitini na sita. Loo, jamani! Hakuna mwandishi ila Mungu Mwenyewe angeweza kuwa sahihi sana. Hakuna Neno moja linalopingana na lingine.

Kumbukeni, miaka elfu moja mia sita mbali mbali, Biblia iliandikwa, tangu Musa hadi—hadi kifo cha—cha Yohana kwenye kile kisiwa, ama Kisiwa cha Patmo. Miaka elfu moja mia sita, na iliandikwa na waandishi arobaini mbalimbali; mmoja hata hakumjua huyo mwingine, nao kamwe hawakuwa nalo kama "Neno." Wengine wao hata hawakuliona "Neno." Lakini wakati walipoliandika Hilo, na ikafahamika kuwa ni manabii, basi, wakati walipounganisha unabii wao pamoja, kila moja ya hizo ilikubaliana na nyingine.

39 Mwangalie Petro, ambaye alitangaza kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu."

Paulo hakuwa amesikia kitu cho chote juu Yake. Alishuka akaenda Arabuni kwa miaka mitatu, kusoma Agano la Kale, kuona kwamba Nguzo hii ya Moto ilikuwa ni nani aliyesema naye njiani, akisema, "Sauli, mbona unaniudhi?" Angewezaje kukosea? Hata hakulitaka shauri kanisa kamwe.

Na miaka kumi na minne baadaye, wakati alipokutana na Petro, walikuwa wakihubiri jambo lile lile, Neno kwa Neno. Hiyo ni Biblia yetu. Hebu maneno ya watu wengine yashindwe. Hili, hakuna mtu anayeweza kuliongeza. Huongezi tena kwenye Biblia. La, bwana. Huu ndio Ufunuo mkamilifu. Ni yote.

40 Kama vile ile Mihuri Saba. "Mihuri Saba," mtu fulani aliendelea kuniambia, "sasa utaninii … Bwana atasema nawe, Ndugu Branham, wakati Mihuri hii itakapofunuliwa, na atatuambia jinsi ya kumkaribia Mungu, na jinsi ya kufanya jambo hilo."

Nikasema, "La, bwana, haiwezi. Kwa sababu, Biblia, ile Mihuri Saba juu Yake ilikuwa imefichwa zile siri saba. Ilikuwa tayari imeandikwa, bali hawakuelewa ilikuwa ni kitu gani."

Angalia jinsi walivyolichimbua jambo hilo, kubatizwa katika Jina la "Yesu"; mnaona, hilo lilikuwa silo. Jina la "Bwana Yesu Kristo"! Angalia mambo hayo yote, jinsi ilivyokuwa. Maana, kuna Yesu wengi; Nina marafiki kadhaa hapa duniani wanaoitwa "Yesu," marafiki wahudumu. Si hivyo. Ni "Bwana Yesu Kristo" wetu.

Hakuna mwandishi ila Mungu angeweza kuwa sahihi sana. Sasa hebu tuone tu jinsi Biblia hii ilivyoandikwa.

41 Sasa, tuseme kwa mfano, kutoka … Vipi kama tungeenda sasa na kuchukua vitabu sitini na sita vya tiba vinavyohusika na mwili, vilivyoandikwa na shule arobaini mbalimbali za matibabu, miaka mia moja na kumi na sita … ama miaka elfu moja mia sita? Sijui tungekuja na mwendelezo wa namna gani?

Wakati, George Washington, rais wetu, yapata miaka mia mbili iliyopita, kwa ajili ya homa ya mapafu, walimng'a ukucha wa kidole chake cha miguu na kumtoa painti moja ya damu. Vipi kama tukichukua …

Hebu tuendelee mbele kidogo, juu ya mambo fulani ambayo tumevutiwa nayo sana siku hizi, ambayo ni sayansi. Vipi kama tungechukua sayansi arobaini mbalimbali, kutoka miaka elfu moja na mia sita, na tuone tutakayoleta? Mwanasayansi Mfaransa, miaka mia tatu iliyopita, alithibitisha kwa sayansi, kwa kuuzungusha mpira, ya kwamba, kama mwendo wowote wa kutisha ulipatikana zaidi ya maili thelathini kwa saa, kitu hicho kingeondoka duniani na kuanguka. Unafikiri sayansi ingeweza kurejea kwenye jambo hilo? Je! Kuna mwendeleo wowote hilo sasa, wakati wanaposafiri barabarani, barabarani hapa, maili mia moja na hamsini kwa saa? Mnaona? Lakini yeye alithibitisha kisayansi kwamba, kwa msukumo wa mpira unaozunguka ardhini, ya kwamba kwa maili thelathini kwa saa, ya kwamba, kitu chochote kingeinuka kutoka duniani na kuondoka, kingeanguka angani. La, hakuna mwendeleo kwa jambo hilo.

42 Lakini hakuna Neno moja katika Biblia linalopingana na lingine. Hakuna nabii hata mmoja aliyempinga huyo mwingine. Walikuwa, kila mmoja, mkamilifu. Na wakati mtu alipoingia na kutoa unabii, na nabii huyo halisi aliinuka na kumwita aje, basi ilidhihirishwa. Mnaona? Mnaona? Kwa hiyo Biblia ni Neno la Mungu, kwa waamini wote wa kweli.

43 Sasa, usingeweza kupata usahihi wowote katika yale madaktari wangekubaliana nayo. Huwezi hata kupata usahihi wake sasa. Huwezi kupata usahihi katika sayansi sasa.

Sasa, mnajua, wakati fulani uliopita, walituambia ya kwamba ninii … ya kwamba, "Wakati Biblia iliposema ya kwamba 'yeye aliwaona Malaika wanne wamesimama katika pembe nne za dunia,' hilo halingewezekana. Dunia ilikuwa mviringo." Lakini Biblia ilisema, "pembe nne." Vema, sasa mmeona, majuma mawili yaliyopita, ama majuma matatu yaliyopita, yamekuwa sasa, magazeti yakiandika makala haya, yaligundua ya kwamba ulimwengu ni mraba. Ni wangapi waliona jambo hilo? Mbona, hakika. Mnaona? Nimeinakili yote, nikingojea tu mtu fulani aseme jambo fulani.

44 Nao wataona, siku moja, ya kwamba hawaoni miaka milioni mia moja na hamsini ya anga la juu. Wanaenda moja kwa moja kwenye duara. Hiyo ni kweli kabisa.

Utatambua, moja ya siku hizi, ya kwamba wakati utakapoenda Mbinguni, hutaruka kwenda mahali pengine. Ungali upo papa hapa, pia, katika kiwango kingine kinachoenda kasi zaidi ya hiki.

Moja kwa moja kwenye chumba hiki kuna rangi inayokuja. Kila rangi, shati, mavazi, cho chote ulichovaa, ni cha Milele, kimewekwa moja kwa moja kwenye rekodi, kikizunguka na kuzunguka ulimwengu. Kila wakati unapofumbua macho yako, ni moja kwa moja kwenye rekodi. Angalia, televisheni itathibitisha jambo hilo.

45 Unapozaliwa, Mungu huweka kumbukumbu. Haileti … Weka rekodi, haileti kelele nyingi kwa muda kidogo, mwajua. Huyo ni mtoto mchanga, mpaka atakapofikia wakati wa kuwajibika; ndipo kelele zinaanza, anaanza kusema mambo na kufanya mambo anayopaswa kuwajibika. Halafu basi wakati huo uhai unapoisha, rekodi hiyo au kanda hiyo inaondolewa na kuwekwa katika—katika maktaba kubwa mno

ya Mungu. Sasa, utauepukaje kwenye ile Hukumu? Unachezwa moja kwa moja mbele yako, kila hatua uliyopiga, kila wazo lililopitia niani mwako. Mnaweza kuona jambo hilo? Sasa unaweza kuona ambapo Mungu …

46 Nikisimama hapa, hivi majuzi usiku, kulikuwako na mtu jukwaani, mtu mrefu, mwenye upara, jamaa mwenye sura nzuri, mwenye nguvu. Naye akatoka … Bwana alikuwa amemwambia mambo mengi sana kuhusu familia yake na yale aliyopaswa kufanya. Naye akatoka akaenda na kuketi chini. Katika dakika chache, hapa alikuja mbele yangu mtu mwingine kama huyo, bali alikuwa ameinamisha kichwa chake. Nisingeweza kugundua, nami nikamwangalia huyo mtu tena huko nje; Naye … Si yeye, kwa sababu ilikuwa ni kitu kingine. Basi mtu huyu, singeweza kupata jambo hilo. Nikaangalia kila mahali, hakuna mtu nyuma, yangu. Nikasema, "Mtu huyo ameketi ndani ya mapazia hayo pale." Na ilikuwa ni ninii yetu … ndugu anayekuja kanisani hapa, mtu mrefu, mwenye upara, na mtu mzuri anayeketi pale namna hiyo. Naye alikuwa ameinamisha kichwa chake juu, akiomba, kwa sababu alikuwa tu karibu kufa kwa ugonjwa wa tumbo.

Alikuwa anaenda kuchukua jozi ya viatu. Mkewe alimtaka anunue jozi mpya ya viatu. Akasema, "La, sina haja ya kuvinunua, kwa maana sitaishi nipate kuvivaa."

Alikuwa anakufa. Naye akiketi pale, unaona, katika kiwango hicho, haleluya, Mungu alisogea tu mle ndani na kusema, "Huyo hapo anaketi," mahali pale pale tu alipokuwa. Mnaona ninalomaanisha?

47 Sasa angalia, na hakuna kosa lo lote katika Maandiko. Yesu, Neno la Mungu, hutambua wazo lililo moyoni. "Neno la Mungu lina nguvu zaidi, ni kali," Waebrania 4:12. "Neno la Mungu ni kali zaidi, lina nguvu zaidi kuliko upanga ukatao kuwili, hata huyatambua mawazo na makusudi ya nia." Mnaona? Unaingia moja kwa moja ndani ya nia, na kuvuta, na kutambua. *Utambuzi* ni nini? "Kujulisha, kufunua." Na hivyo ndivyo Neno la Mungu linavyofanya.

Leo tunasema, "Kanisa Katoliki ni Neno la Mungu; Wabaptisti, Wamethodisti, Wapentekoste, maskani." Hilo ni kosa. Neno ni ufunuo; Mungu, akifunuliwa kwa Neno.

48 La, tungelipata … kupata mwendeleo wowote miongoni mwa madaktari, miongoni mwa wanasayansi, watu mbalimbali.

Laiti Einstein angalikuwa na matumizi ya kiroho, kama vile alivyokuwa na—na matumizi ya maumbile, wakati alipokuwa anajifunza kanuni za nuru, na kadhalika, yeye angaliweza kutuambia kitu fulani. Niliposikia ujumbe wake juu ya mahali pale pa katikati mahali fulani katika anga, ya kwamba, "Ukiwahi kuwasiliana na mahali hapo pa katikati, ungeweza kuumba dunia, kufanya jambo lo lote, na hizo nguvu zisingekuwa na mpaka." Mnaona? Alikuwa ameona jambo hilo.

49 Unaona vijifuko hivi vinavyopita hewani, wanaviita "visahani," na kadhalika. Watu hivyo … Hicho, vema, afadhali tuachilie mbali jambo hilo. "Mmesikia watu hawa wote ambao wamekosekana?" Hatusikii habari zao; wao wamesimama hapo, halafu hawako.

Hivyo ndivyo Unyakuo utakavyokuwa. Kimoja cha hivyo kitashuka moja kwa moja, na huu mwili wa duniani utachukua wa kimbinguni. Nao watakuwa…ngozi, nywele, ama mifupa itakayosalia; vitabadilishwa katika dakika moja, kikishuka moja kwa moja kutoka angani na kuuchukua huo nyumbani. Tunaona haya yote yakiendelea sasa, na ile—na Pentagon ikishangaa kuhusu taa hizi, na nuru za kisiri, na kila kitu wanachokiona angani. Umeona walikuwa na moja hapa kwenye gazeti huko Jeffersonville juma hili, na kadhalika, "nuru ya kisiri." Kwa hiyo, loo, hawajui hiyo ni nini. Lakini sikilizeni, enyi watoto wadogo, itawachukua, moja ya siku hizi. Mnaona? Mnaona? Usijali.

Kumbukeni, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma."

50 Ni kitu gani kilichotukia kabla tu ya Sodoma? Mungu alishuka pamoja na baadhi ya Malaika , nao walikuwa na hukumu ya upelelezi. Kasema, "Nimesikia kilio, ambacho ni cha dhambi sana, kikuu sana, kwa hiyo nimeshuka kuchunguza kwa jumla kama ni kweli au si kweli." Hiyo ni kweli? Mwangalie yule Mmoja aliyebaki na Ibrahimu, angeweza kutambua mawazo yaliyokuwa katika moyo wa Sara, nyuma Yake.

Sasa, hebu angalia kila mahali kidogo tu na uone, unaona, angalia kile inachofanya, jambo lile lile leo. Ni hukumu ya upelelezi.

Mbona, baada ya kitambo kidogo, Kanisa, wakati linapoweza kukaa mahali hapo, na kila mbegu imeletwa mahali pake, watakuwa wamekwenda. Hawatajua kilichowapata. Mmoja atakuwa akienda upande mmoja. Mnaona? Mmoja atakuwa anaenda kwenye nyumba ya mchungaji, na mmoja atakuwa anaenda hapa, ama kule chini, halafu, muda si muda, wao hawako. Kwa kuwa Henoko aliyekuwa ndiye mfano, "Mungu alimchukua, naye hakuonekana." Wanashuka kuja kupeleleza! Huo mwendeleo, jinsi kule kubadilishwa kwa Henoko, mfano. Wa Israeli kuchukuliwa juu katika ile safina…

51 Ni kamilifu sana, Neno la Mungu ni kamilifu sana, hata kwa Agano la Kale na Agano Jipya, ni nusu

mbili na moja nzima. Hiyo ni kweli. Agano la Kale ni nusu Yake, na Agano Jipya ni nusu Yake; ukiliweka pamoja, una ufunuo wote wa Yesu Kristo. Hao hapo manabii wakinena, na huyu hapa katika Mwili; mnaona, nusu mbili na moja nzima. Sasa hatutaki kuchukua mengi mno …

52 Sasa, kumbukeni, Agano la Kale si kamili bila lile Jipya. Na lile Jipya lisingeweza kuwa kamilifu bila ya lile la Kale. Hiyo ndiyo sababu nilisema nusu mbili, moja nzima. Kwa kuwa, manabii walisema, "Atakuwa hapa! Atakuwa hapa! Atakuwa hapa; watamfanyia *hivi*. Watamfanyia *hivi*!" Naye ndiye huyu hapa, "Alikuwa hapa! Yeye alikuwa hapa, nao walimtendea *hili*, nao walimtendea *hili*." Nilihubiri tu jambo hilo siku chache zilizopita usiku.

53 Sasa, kusudi tupate kusoma Maandiko, Paulo alimwambia Timotheo, "Jifunze, ukitumia kwa halali Neno la Mungu, ambalo ni Kweli."

Hayo ni matakwa matatu katika Maandiko. Katika kutumia Neno la Mungu, kuna mambo matatu ambayo hupaswi kufanya. Sasa hebu na tusome hayo kwa dakika kumi zifuatazo; mambo matatu ambayo hupaswi kufanya. Na ninyi nyote mlio nchini, popote mlipo, kote nchini, hakikisheni mnaweka haya moyoni mwenu kama hamna penseli. Haikupasi kufanya mambo haya. Tunawaambia wakati wote jinsi mnavyopaswa kufanya, sasa nitawaambia yale msiyopaswa kufanya.

Sasa, hupaswi *kulifasiri* Neno vibaya. Unasema, "Vema, ninaamini inamaanisha *hivi*." Linamaanisha vile tu linavyosema. Halihitaji mfasiri. Wala hupaswi *kuliweka* Neno *mahali pasipo pake*. Wala hupaswi kuliweka Neno mahali pasipo pake. Na kama tukifanya moja ya mambo katika haya, jambo hilo litatupa Biblia nzima katika mchafuko na ghasia.

54 Angalia. Kumfasiri vibaya Yesu, katika mfano wa Mungu katika mwanadamu, ungemfanya—ungemfanya Yeye Mungu mmoja kutoka kwa watatu. Kumfasiri vibaya Yesu Kristo akiwa ni Neno, ungemfanya Yeye Mungu mmoja kati ya watatu, la sivyo ungemfanya Yeye Nafsi ya pili katika Uungu. Na kufanya hivyo, ungevuruga Maandiko yote. Usingeweza kufika po pote. Kwa hiyo halipaswi kufasiriwa vibaya.

Na kama ukisema ya kwamba jambo fulani, ukiweka fasiri fulani juu Yake, na kulitumia Hilo kwa wakati mwingine; ama limekwisha kutumiwa kwa wakati mwingine, unafanya fasiri isiyo sahihi pia.

55 Kama mtu ye yote akimfasiri vibaya Yesu Kristo katika Biblia, ya kumfanya Yeye si Mungu Mwenyewe, kumfanya Yeye Nafsi ya pili, ama Mungu mmoja kati ya watatu, hii ingevuruga kila Neno katika Biblia nzima. Ingevunja amri ya kwanza, "Usiwe na mungu mwingine ila Mimi." Vema. Ingefanya jamii yote ya Kikristo kundi la waabudu wapagani wakiabudu miungu watatu mbalimbali. Mnaona mngekuwa na Biblia ya namna gani? Ndipo lingetufanya sisi kuwa kile ambacho Wayahudi wanasema tulicho. Kasema, "Ni yupi kati ya hao miungu aliye Mungu wenu?" Mnaona? Kwa hiyo, mnaona, huwezi … Hampaswi kuifasiri Biblia vibaya.

Kwa kuwa, Yesu Mwenyewe ndiye fasiri ya Biblia, wakati anapodhihirishwa katika wakati ambapo sehemu ya Mwili Wake inadhihirishwa. Kama ni wakati wa mkono, lazima uwe mkono; hauwezi kuwa wakati wa kichwa. Kama ni wakati wa sauti, vema, basi, haiwezi kuwa ni wakati wa miguu. Mnaona? Na sasa tuko kwenye wakati wa macho. Na sasa kinachofuata, ni Yeye Mwenyewe, kuja. Kuona; ya kinabii!

56 Mnaona, kote katika wakati, tulianza kutoka kwenye msingi, kutoka kwenye wakati wa kwanza wa kanisa; wakati ile Mbegu ilipoingia ardhini, ile Mbegu kamili. Ndipo ikatokea kwa miguu, Luther; kurudi tena kupitia kwa Wesley; halafu kwa Wapentekoste, lugha, katika midomo, mnaona; sasa ni katika macho, ya kinabii, ya Malaki 4, na kadhalika. Na sasa hakuna kitu kingine kilichosalia kuja ila Yeye Mwenyewe kuingilia jambo hilo, maana hilo ndilo jambo la mwisho lililopo.

Ifuatayo ni akili, wala hatuna akili zetu wenyewe; ni Yake. Hatuna macho yetu wenyewe. Mtu anawezaje kuona mambo hayo kimbele? Hawezi kufanya hivyo. Ni Mungu Mwenyewe. Unaona, inafaa—inafikia mahali fulani. Naye ameutawala mwili kote kote, ndipo Mwili mkamilifu wa Kristo unafunuliwa katika umbo la Bibi-arusi aliyeondolewa ubavuni Mwake, kama Adamu alivyofanya hapo mwanzo … kama vile alivyokuwa Adamu, hasa, hapo mwanzo.

57 Naam, "mungu," hii ingeitia Biblia nzima katika mchafuko, kuvunja amri ya kwanza, na kumfanya mungu, mungu wa kipagani wa watatu. Inge—ingeharibu tu picha nzima ya Biblia. Kwa hiyo hupaswi kuifasiri vibaya Biblia. Sasa, hilo ni jambo moja tu.

Wakati, kila Andiko katika Biblia lina matumizi yale yale, huna budi kuliweka mahali Pake. Na kuliweka mahali pasipo pake, huenda ukamfanya Mungu katika wakati mmoja, na—na wakati ufuatao ungemfanya Yeye historia, kuliweka Hilo mahali pasipo pake. Kwa hiyo hupaswi kuyaweka Maandiko mahali pasipo pake. Yeye ni Mungu wakati wote. Kama ulimfanya leo kuwa Mungu wa historia, kile kilichokuwa huko nyuma, Naye si yeye yule leo, utafanya nini na Waebrania 13:8? Mnaona, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

Sasa, kwa hiyo angalieni jambo hili lingefanya nini, na vile limefanya. Tayari limefanya jambo hilo, kumfanya akane Neno Lake Mwenyewe, kuweka Maandiko mahali pasipo pake.

58 Kuondoa Maandiko, huenda ukauweka mwili Wake pamoja vibaya, mguu mahali ambapo kichwa kinapaswa kuwa, ama kitu fulani. Ni kama tu … Kwa maneno mengine, huenda ukawa na Yesu akifundisha ujumbe wa Musa. Huenda ukawa na … ama hata Wesley akifundisha wakati wa Luther. Huenda ukawa na sasa, wakati wetu, ukifundisha Pentekoste, ujumbe wa Kipentekoste. Mnaona ingekuwa mchafuko gani? Pentekoste tayari imeonyesha rangi zake. Luther tayari ameonyesha yake, akaingia katika madhehebu. Ilikufa papo hapo. Wakati huo ukawadia; ukaisha.

Angalia, mara tu ilipounda madhehebu, ilikufa. Sasa, angalia tu kama hiyo si kweli. Angalia huko nyuma katika kurasa za historia. Kila wakati lilipounda madhehebu, lilikufa papo hapo; hakukuwako tena na jambo hilo. Lilifanyika mwa—mwabudu wa mungu wa dunia hii, na kuingia katika matengenezo, na mashirika, na madhehebu, na madanganyo. Kundi la akina Ricky waliingia mle na kuweka pingamizi zao wenyewe ndani yake, ama waliingiza mawazo yao wenyewe, hasa, ndani yake. Na lilitukiaje? Ukawa mchafuko. Wakielekea kwenye mungu wa ulimwengu huu, ambapo watamtawaza Shetani mwenyewe, wakifikiri ya kwamba wana kiongozi mkuu wa ulimwengu awaletee amani.

59 Niliwaambia hivi majuzi, nitalisema tena, ya kwamba hata ustaarabu wenyewe leo hii ni kinyume kabisa cha Mungu. Ustaarabu ni kinyume cha Mungu. Elimu ni maili milioni moja kutoka Kwake; sayansi ni maili milioni moja. Sayansi na elimu vinajaribu kumkana Mungu, mnaona, kupitia kwenye seminari za kitheolojia na shule, na vyumba vya sayansi, na kadhalika. Wamekuwa na mtikiso wao.

Vipi kuhusu lile ono usiku wa juzijuzi, la mtu yule wakati alipowapigia makelele wale wanasayansi kule chini wakimwaga vitu hivyo namna hiyo? Waligeuka tu na kuangalia juu, kisha wakaendelea. Kutakuwa na kupanda farasi mara nyingine tena.

60 Angalia, loo, mambo haya matatu hayana budi kuwa. Sasa, huwezi … Yesu hakuja akihubiri ujumbe wa Nuhu. Yeye hakuja akihubiri ujumbe wa Musa. Ama, Musa hakuja akihubiri … Mnaona, msiyaelekeze Maandiko sehemu isiyo yake. Haina budi kuwa katika wakati huo. Sasa, huwezi kutumia … Wakati mtu huyo mashuhuri, John Wesley, alipotoka, ama …

Yule mtu mashuhuri, Luther, wakati Luther alipotoka na ujumbe wake wa kuhesabiwa haki. Sasa wakati huo ulikuwa … Luther alikuwa mtu mashuhuri. Yeye aliliita kanisa litoke gizani, naye akaweka kuhesabiwa haki kwa imani. Na wakati alipofanya jambo hilo, walijenga dhehebu juu yake, nalo likafa. Ule Uzima ulisafiri, kama ulivyo katika shina la ngano, moja kwa moja kwenye wakati wa Wesley, kwenye kishada. Kutoka kwa Luther yakaja majani mengine, ambayo yalikufa pamoja nao, ambayo yalikuwa Zwingli, na Calvini, na hao wengine wote waliotoka kwenye hayo matengenezo makuu.

61 Ndipo baadaye akaja Wesley, wakati mwingine ulikuwa umechanua na kuwa kishada. Wesley, na Atterbury, na hao wote, na—na John na ndugu yake, na hao wote, watu mashuhuri wa Mungu wakiwa na ujumbe, waliueneza nchini. Wakalifanya madhehebu; likakufa.

Ndipo ikatokea ikionekana kabisa kama tu vile ilivyokuwa ikienda kutoa punje sasa, na, ikaja kutambua, ilikuwa ni kapi, Pentekoste.

Lakini huko nyuma nyuma ya hayo yote, kukaja chipukizi dogo.

Nanyi mnaona, kwa kawaida … Nafikiri, katika yapata miaka mitatu ama minne baada ya Luther kuwa kazini, ya kwamba kanisa la Kiluteri liliunda madhehebu. Muda mfupi tu baada ya Wesley kuwa uwanjani, lilifanywa dhehebu.

62 Tucson, tumekuwa na—na mpango wa jinsi kanisa la Wesley, ama kanisa la Kimethodisti, lilivyopatikana. Na walipokuja Marekani hapa, wengi wao walikuwa wamerudi na kusema walikuwa wameunda ka—mkataba na kadhalika, kutoka Uingereza, kuuleta hapa, na jinsi yote yalivyoigizwa. Niliona papo hapo kile kilichotukia. Na hapo likafa.

Vema, wakatoka Wapentekoste, hao wapiga makelele wa kale huko nyuma katika siku nyingi zilizopita, wakiwa na karama ya kunena kwa lugha, wakaanza kwa kunena kwa lugha. Ndipo wakaliita jambo hilo, "ushahidi wa Roho Mtakatifu." Ndipo wakaunda madhehebu. Mmoja akasema atafanya *hivi*, na mwingine *vile*, nao walikuwa na visa na visa. Lilifanya nini? Kila moja ya majani hayo yanafunuliwa tu, kama tu vile yalivyofanya kwenye shina na kama yalivyofanya kwenye kishada. Walikuwa na umoja, uwili, utatu, na kanisa la Mungu, na haya mengine yote; ilifunuliwa tu, imefunuliwa, imefunuliwa.

Lakini sasa, kulingana na maumbile ya asili, ambayo ni kielelezo kikamilifu, hutakuwa cho chote cha kulielimisha Hilo litoke mle

63 Jamaa fulani, ya rafiki zangu kule Kentucky, ndiyo kwanza wapate mtoto m—mchanga aliyezaliwa juzijuzi, na mama alikuwa ameamka walipokuwa wakitupikia chakula cha jioni. Naye alikuwa akimsaidia

yule dada mwingine kulipikia chakula kundi letu sisi wanaume tuliokuwa tumetoka mawindoni. Na kwa hiyo mtoto huyo akaanza kulia, nami nilikuwa nikizungumza. Nafikiri mama aliona aibu kidogo, kwa hiyo akakimbia na kumchukua mtoto huyo, na—na kuanza ku—kumlisha jamaa huyo mdogo. Nikasema, "Unajua, hayo ni maumbile asili tu." Mnaona? Sasa, huwezi …

Hawajawahi kupata njia bora zaidi kwa mtoto mchanga kupata kile anachotaka kuliko kukililia. Sasa, huenda ukakipa ki—kitabu cha maadili, na kuketi hapa chini na kusema, "Ninataka kukufundisha theolojia, mwanangu. Sasa, msije mkapiga mayowe hapa kama watoto wengine; wewe ni tofauti. Sasa, unapotaka kulishwa, piga kengele hii ndogo hapa." Haifai tu kitu. La, haifai kitu.

64 Kwa hiyo, unapoangalia maumbile ya asili, sasa tunaona mahali kila wakati, na moja kwa moja inaonyesha wazi ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho. Kapi limeondoka. Nasi tumekuwa na miaka kumi na mitano, karibu ishirini sasa, miaka, ya huu Ujumbe kuenea kutoka taifa hadi taifa, na asubuhi ya leo tumeunganishwa kwa simu na kila mahali nchini humu, mnaona, na hamna madhehebu. Hauwezi kuunda madhehebu. Hakuna kitu kilichowahi kuwa kama hicho, ama kitakachokuwa baadaye. Mnaona?

Ki—kitu ambacho kinahusika na Ujumbe leo, ni, wale wanaoupokea mioyoni mwao hawana budi kukaa katika Uwepo wa Mwana, wapate kuiva. Mnaona? Unaweza kuutwaa Ujumbe, halafu umwache Mwana aukaushe ubichi wote ukutoke, amfanye Wakristo waliokomaa. Mnaona ninalomaanisha? Mungu yuaja hivi karibuni, kulipokea Kanisa Lake, nasi hatuna budi kuwa na Wakristo wa aina hiyo apate kuwapokea. I—ngano haina budi kukomaa. Vema.

65 Haya masharti matatu hayana budi kuwa. Haipaswi kufasiri vibaya, ama kulitumia vibaya, kulifasiri Hilo, ama ku—au kuliondoa kwenye sehemu Yake. Halina budi kuwekwa sawa kabisa jinsi Mungu alivyosema ilikuwa.

Kwa ulimwengu, ni Kitabu cha fumbo. Watu wanaamini ni Kitabu cha kimafumbo tu. Wakati mmoja nilikuwa nikizungumza na mtu mashuhuri sana hapa mjini, ambaye ana msimamo mkuu wa Ukristo, naye akasema, "Nilijaribu kusoma Kitabu cha Ufunuo usiku mmoja." Kasema, "Yohana hapana budi alikuwa amekula masarufu ya pilipili kali kisha akapata jinamizi." Mnaona, Kitabu cha siri.

66 Lakini, wakati kwa mwamini wa kweli, ni ufunuo wa Mungu akifunuliwa katika wakati tunaoishi. Yeye alisema, "Maneno Yangu ni Roho na ni Uzima." Yesu alisema hivyo. Tena, "Neno ni Mbegu ambayo mpanzi alipanda." Tunajua ya kwamba hiyo ni kweli. Ni Mungu katika umbo la Neno, na anaweza tu kufasiriwa na Yeye Mwenyewe.

Akili ya mwanadamu haiwezi kufasiri nia ya Mungu. Mtu mdogo—mwenye kikomo anawezaje kufasiri Akili isiyo na kikomo, wakati hatuwezi hata kufasiri mawazo ya mtu mwingine?

Nanyi mnaona, Yeye Ndiye pekee anayeweza kulifasiri, Naye analifasiri kwa Yeye atakaye. Haikusema, "Wanadamu wa kale, walipokuwa wakizunguka-zunguka duniani katika nyakati nyingi na kwa namna nyingi." "Mungu, katika nyakati nyingi na kwa njia mbalimbali alijifunua Mwenyewe kwa manabii Wake." Mnaona?

67 Na, angalia, "Kwa yule Yeye atakayemfunulia Hilo." Naye alibuni sana hata anaweza kujificha Mwenyewe katika Maandiko, kwa mwanatheolojia mwenye akili sana aliyeko. Loo, jamani! Yeye anaweza tu kujificha, akakaa papo hapo katika Maandiko, nawe unaangalia siku nzima usione jambo hilo; angalia maisha yake yote, wala usione kamwe. Anaweza tu kujificha, akiwa pale.

Sasa, tafadhalini, kila mahali, jalia hilo liingie ndani. Kwamba, Mungu, katika Neno, anaweza kujificha Mwenyewe sana katika Neno, hata hakuna mwanatheolojia wala shule ulimwenguni inayoweza kumpata, na hata hivyo ameketi papo hapo.

Unasema, "Hiyo ni kweli, Ndugu Branham?"

Vipi kuhusu Mafarisayo na Masadukayo? Vipi kuhusu katika kila wakati? Yeye amefanya jambo hilo. Hakika. Yeye amefanya hivyo katika kila wakati. Sasa tungeweza kuangalia hilo. Hebu na tufikirie juu ya siku za Nuhu; wakati mzuri, wa kielimu, jinsi alivyojificha katika Neno Lake lililoahidiwa. Katika siku za Musa, jinsi alivyojificha. Katika siku za Eliya, jinsi alivyojificha. Katika siku za Yesu, jinsi alivyojificha. "Alikuwa ulimwenguni, na ulimwengu uliumbwa kwa Yeye, wala ulimwengu haukumtambua. Yeye alikuja kwa walio Wake; Walio Wake hawakumpokea." Mnaona?

68 Yeye hujificha kutoka kwa mtu mwerevu sana, mtu mwenye elimu aliyeko duniani. Unasema, "Vema, huyu ni Dk. Baba Mtakatifu Fulani." Sijali yeye ni nani, Mungu hujificha kutoka kwake; na atawafunulia watoto wachanga ambao watajifunza, mnaona, watoto wa Mungu, mbegu zilizochaguliwa tangu asili.

Wazia. Mungu Mwenye Nguvu, akiketi katika Maneno Yake Mwenyewe, akiwapofusha watu werevu, wenye elimu wa wakati huu wa sasa, nao hawaoni jambo hilo. Wanafikiri ni kundi tu la ushupavu wa dini. Mwangalie Yeye amesimama pale akijificha, kwa Wapentekoste, Wabatisti, Wamethodisti, Wapresbiteri.

Kujifunua Mwenyewe moja kwa moja hadharani, na kuonyesha kila namna ya mambo, hata kuyaweka kwenye magazeti, na mambo kama hayo, hata hivyo hawalioni. Loo, Mungu wetu, namna alivyo mkuu, akijifunua Mwenyewe kwa ye yote atakaye.

“Loo,” unasema, “Ndugu Jones ama Ndugu Nanii, yeye ni—yeye ni mtu mashuhuri. Yeye ataiona.” Loo, la. Yeye humfunulia Yeye amtakaye. Sema, “Mke wangu halioni Hilo, naye ni mwanamke Mkristo.” Yeye hujifunua kwa kila mtu amtakaye. “Vema, mchungaji wangu ni mtu mashuhuri.” Hiyo ni kweli, bali Yeye hujifunua kwa Yeye atakaye. Sasa, chunguza na yale yaliyofunuliwa, kwa yale yanayotendeka, ndipo utaninii … unaweza kuelewa kabisa.

69 Sasa tunaona basi, inalifanya Kitabu cha Mungu na si kitabu cha mwanadamu. Kama lilikuwa ni la mwanadamu … Sasa hebu tuangalie jinsi lingejieleza Lenyewe. Angalia jinsi inavyoficha dhambi ya watu walioliandika, angalia, watu ambao—ambao waliishi katika siku Zake.

Ibrahimu, kwa mfano, yeye anaitwa “baba wa waaminifu.” Angalia jinsi ambavyo … Unafikiri Ibrahimu angeandika Kitabu hiki juu ya nafsi yake, kuhusu woga wake mwenyewe? Namna unavyofikiri angeandika ya kwamba alimdanganya mfalme asubuhi hiyo, na kusema huyo alikuwa ni dada yake, wakati alikuwa ni mkewe? Ingeandikwa juu ya matendo yake ya uoga aliyofanya? Hakika, asingefanya hivyo kamwe.

Vipi kuhusu Yakobo katika udanganyifu wake? Maskini mdanganyifu ambaye Yakobo alikuwa. M—m—mtu angeweza, Mwebrania akiandika juu ya ndugu yake Mwebrania, ambaye katika yeye Israeli yote iliitwa jina, hivi angethubutu kuandika udanganyifu wa baba halisi wa taifa zima? Katika Yakobo, walitokea wale wazee wetu; kutoka kwa wale wazee wetu, makabila yakatokea. Na jiwe la msingi la hayo yote, Biblia inamfunua kama mdanganyifu. Hiyo ni kweli? Unafikiri mwanadamu angeandika hayo? La, bwana.

70 Vipi kuhusu mtu kuandika juu ya mfalme mkuu sana waliyepata kuwa naye hapa duniani, kama mfalme aliyevikwa taji; Daudi, katika kufanya uzinzi wake? Je! Hao Wayahudi wangewahi kuandika juu ya mfalme wao aliye bora sana kuwa mzinzi?

Loo, tuna historia, kama, “George Washington hakusema uongo kamwe,” na mambo kama hayo. Tunasema, tutaita historia hiyo.

Lakini huyu ni mwanadamu, Biblia inayomwita Daudi “mzinzi,” naye alikuwa hivyo. Mfalme wa Israeli, mzinzi ambaye angekuwa mwana … Yesu awe Mwana wa Daudi. Jiwe la msingi kabisa; na baba Yake, kulingana na mwili, alikuwa mzinzi. Wayahudi kamwe wasingeandika Kitabu kama hicho. Je! Mwanadamu angeandika haya kwa nafsi yake? Bila shaka sivyo.

71 Taifa hilo la Israeli lenye kiburi lingewezaje? Unajua jinsi walivyojivuna. Taifa lenye kiburi la Israeli, lilikwenda na kuandika juu ya ibada zao za sanamu, liliandika juu ya uasi wao dhidi ya Mungu wao, liliandika dhidi ya mambo machafu, machafu waliyofanya, na kuandika katika kitabu? Bila shaka wangeficha jambo hilo. Wangalionyesha tu mambo mazuri. Lakini, Biblia hii, inayosema yaliyo mema na mabaya. Ni, kila mtu anajua ya kwamba Wayahudi kamwe wasingeandika Kitabu kama hicho, kuhusu uchafu wao wenyewe, na ibada ya sanamu, na kushindwa, na kila kitu walichokuwa nacho. Wasingeandika hayo kamwe. Loo, la.

Halafu, ni Nani aliyeliandika? Biblia ilisema, katika Waebrania 1:1, “Mungu alisema na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi.” Halafu, haikuwa ni manabii, haikuwa ya kibinadamu. “Mungu!” Si “manabii katika siku nyingi.” Lakini, “Mungu, katika siku nyingi, kwa njia nyingi alinena na baba zetu kwa njia ya manabii.”

Nina Andiko lililoandikwa hapa. Sijui ni kitu gani; Siwezi kulitaja. Kwa kawaida, wakati mambo haya ninayotaja, ninaangalia Maandiko. Nitaangalia kwa dakika moja tu, kama mtanisamehe. Ni Timotheo wa Pili 3:16. Ni—ni—nilifikiri ningekumbuka jambo hilo, lakini ninasikitika. Nitasimama kwa dakika moja tu kujua ni kitu gani.

72 “Mungu, zamani za kale na kwa njia nyingi alinena na baba zetu kupitia manabii.”

Sasa Timotheo wa Pili 3, 3:16. Hebu tuone kile inachosema katika 3:16.

> *Kila andiko* (ndiyo), *lenye pumzi ya Mungu* (Manabii? La) ... *pumzi* (Nini?) *ya Mungu*, *lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki;*
>
> *IIi mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*

Vema, basi, Maandiko yote yameandikwa kwa uvuvio. Yesu, hapa duniani, alisema ya kwamba mbingu na nchi zitapita, bali Neno Lake halitapita. Yeye alisema Maandiko yote hayana budi kutimizwa. Kwa hiyo basi Kitabu hicho si kitabu cha maandishi ya mwanadamu. Ni Vitabu vya maandiko ya Mungu.

73 Sasa, tunajua Mungu alichagua kwa kuchagua tangu asili Kanisa Lake, mahali Pake, manabii Wake, na yote kuhusu jambo hilo. Kwa kujua tangu asili, Yeye alimchagua tangu zamani nabii Wake. Na ule wakati ulipowadia, Yeye alimfanya nabii Wake awasili wakati uo huo, na kumvuvia jinsi alivyoiandika Biblia kwa huyo. Sasa, Mungu aliandika Biblia kwa kutumia tu nabii, kwa sababu hiyo ndiyo njia Yake ya kufanya jambo hilo. Kwa hiyo, mnaona, si neno … Kwa hiyo, mnaona, ni Neno la Mungu, na si neno la mwanadamu.

74 Mungu ni Mtu. Mungu anaweza kunena. Mungu anaweza kuzungumza. Mungu anaweza kuandika. Haikumlazimu kufanya jambo hilo namna hiyo, bali hivyo ndivyo Yeye—Yeye alivyochagua kulifanya. Haikumlazimu kulifanya namna hiyo, bali alichagua kulifanya namna hiyo. Sasa unasema, "Mungu aliandika kwa kidole Chake, kidole Chake Mwenyewe, zile amri kumi. Kwa hiyo Mungu angeweza kuandika, Yeye Mwenyewe kitukufu, kama alitaka kuandika." Mnaona? Lakini Yeye—Yeye alichagua kuliandika kupitia kwa manabii, mnaona. Kwa sababu ilikuwa ni sifa Zake, Neno Lake, Yeye alilidhihirisha kupitia kwao, akifanya yote kuwa sehemu, ama sehemu Yake. Mnaona? Angeweza kuandika kwa kidole Chake. Yeye pia alichukua kidole Chake na kuandika juu ya kuta za Babeli, "Umepimwa katika mizani ukaonekana umepunguwa." Yeye aliandika kwa kidole Chake Mwenyewe.

75 Mungu anaweza kuzungumza. Unaamini Mungu anaweza kuzungumza? Alizungumza na Musa mlimani, kwenye kichaka kilichowaka moto. Unaamini jambo hilo? Naam, bwana. Yeye alinena na Yohana, katika umbo la hua, (mnaamini hilo?) Ya kwamba, "Huyu ni Mwanangu mpendwa Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake." Alizungumza naye. Yeye alinena na Yesu juu ya Mlima wa Kugeuzwa, mbele ya Petro, Yakobo, na Yohana. Anaweza kuzungumza. Yeye si bubu. Mungu anaweza kuzungumza. Kwa hiyo Yeye alinena na—na Yesu kwenye Mlima wa Kugeuzwa Sura. Naye alinena na Yesu mbele ya umati wa watu; wakati, watu walisema ilinguruma, bali ilikuwa ni Mungu akinena na Yesu. Na karibu Mathayo yote, Marko, Luka, na Yohana, ni Yesu akinena. Yeye ni Mungu. Kwa hiyo, Mungu anaweza kuzungumza.

76 Akachukua vidole Vyake Mwenyewe na kuandika juu ya mchanga, siku moja. Yeye alinena, alihubiri, alitabiri, kwa midomo Yake Mwenyewe, Mungu alifanya hivyo, wakati alipofanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, "Mungu akidhihirishwa katika mwili." Kama anaweza kuandika, kunena, hawezi pia kuwaambia wengine wafanye nini? Hakika anaweza. Anaweza kuzungumza nao, katika sauti ya kibinadamu. Anaweza kuandika na kuwaonyesha la kufanya. Yeye amefanya hivyo.

Kwa hiyo, "Mungu, zamani za kale na kwa njia nyingi alinena na baba zetu kupitia manabii." Naye akasema, katika Maandiko haya, ya kwamba, "Hakuna hata yodi moja wala nukta moja itakayopita hata limetimia," halafu linadhihirishwa; kisha litatimia, kwa maana limedhihirishwa. Haiwezi kupita wakati huo, bali Neno Lenyewe linafanyika mwili. Yodi maana yake ni "neno dogo." *Nukta* maana yake ni "alama ndogo." Si hata kituo kimoja, tamshi moja, cho chote, kitakachoshindwa katika Neno la Mungu. Haiwezi kushindwa, kwa sababu ni Mungu, Mungu aliyedhihirishwa katika umbo la mwili wa mwanadamu. Kwa kuwa, ni Mungu Mwenyewe katika umbo la barua, umbo la nabii, aliyedhihirishwa katika mwili.

Sasa hiyo, ndiyo sababu Yesu aliweza kusema, "Wale walionena nanyi, mnawaita 'miungu,' walionena nanyi kwa Neno la Mungu," kasema, "nao walikuwa miungu." Hao manabii walipotiwa mafuta na Roho wa Mungu, na kuleta Neno la Mungu hasa, basi walikuwa miungu. Ilikuwa ni Neno la Mungu likinena kupitia kwao. Na unaweza …

77 Wanafasiri tu kama vile Mwandishi angewaruhusu kufasiri. Sasa kama unataka kupata jambo hilo, hiyo ni Petro wa Pili 1:20 na 21. Vema. Maana, hapa, ambapo Mungu … "Hakuna mfasiri wa kibinafsi." Yeye hujifasiria Mwenyewe.

Mungu hunena na kulifasiri Hilo, Mwenyewe, kisha hulifunua kwa yeyote atakaye, huwaficha wengine wote. Yeye haimlazimu kumfunulia mtu awaye yote isipokuwa awe anataka kufanya hivyo. Na Yeye haninii … Yeye, Yeye ameelezea jambo Lake lote katika Maandiko, kwa hiyo jambo hilo lote tayari limejulikana; ni Yeye tu ameketi pale akiliona likitukia. Mnaona? La. Kuona tu ule Mwili ukifanywa na kurudi kwenye Wake, katika umbo, Bibi-arusi Wake tena. Vema.

78 Waamini wanaliamini, kama vile Ibrahimu aliyeyaita mambo kinyume Nalo kana kwamba hayakuwapo.

Pia, Neno hili, hutambua siri za mioyo, Waebrania 4:12. "Hutambua siri za moyo."

79 Manabii sikuzote hawakuelewa yale waliyokuwa wakiandika ama yale waliyokuwa wakisema, la sivyo wasingeweza kuyasema, kama wangeweza kuyaelewa. Mnaona? Lakini Biblia ilisema, "Waliongozwa na Roho Mtakatifu." Waliongozwa! Wakati Roho Mtakatifu anapokuongoza, nenda. Mwanadamu … "Mungu, zamani za kale na kwa njia nyingi aliwaambia manabii waliosukumwa na Roho Mtakatifu." Hiyo ndiyo sababu, katika nyakati zote, watu waliokuwa wa kiroho waliwataka shauri manabii juu ya nyakati na yale yaliyokuwa yatokee.

Nabii-mwandishi hana budi kuwa katika ushirika wa daima na Mwandishi. Mnaona? Hana budi kuishi daima Mbele za Mwandishi, kujua vile Kitabu kitakavyokuwa. Mnaona? Yule nabii-mwandishi, alikuwa na

kalamu tayari wakati wo wote, ushirika wa daima na Mwandishi, ambaye alikuwa ni Mungu, kuandika kila alichosema aandike. Mnaona? Alionyesha ni maisha ya aina gani anayopaswa … maisha yaliyotengwa na ndugu zake wote.

80 Sasa, hiyo ndiyo sababu nabii aliweka nia yake daima juu ya yale Mungu aliyosema; si kile mwanadamu alichowazia, kile ambacho wakati ulifikiri, kile kanisa lilichowazia, kile ufalme ulichowazia. Kile Mungu alichowazia! Yeye alielezea tu mawazo ya Mungu kwa Neno, maana neno ni wazo linapotamkwa. Mmelipata sasa? Neno ni wazo lililotamkwa, kwa hiyo nabii alikuwa akingojea mawazo ya Mungu. Na wakati Mungu alipomfunulia mawazo Yake, aliyaeleza katika Neno, "BWANA ASEMA HIVI." Mnaona, si "Mimi, nabii, nasema hivi." "BWANA ASEMA HIVI!" Mnaona? Vema.

Hiyo ndiyo sababu wao waliziasi falme na nyakati za kanisa, ambapo, kufanya jambo hilo katika siku zao, ilikuwa ni ni hukumu ya kifo. Unatembea katika uso wa mfalme na kumwambia, "BWANA ASEMA HIVI, hivi na vile vitatukia," ungekatwa kichwa chako. Kanisa lingekuua sasa hivi kwa kufanya jambo hilo. Lakini manabii hawa walikuwa wajasiri. Kwa nini? Wao waliongozwa na Roho Mtakatifu, mnaona, na, wao, hiyo ndiyo sababu walipata ujasiri. Nao waliandika Ne—Neno la Mungu lisilokosea.

81 Kulikuwa na wengi waliojaribu kuwaiga hao manabii, kama makuhani, ama kadhalika. Nao walifanya nini? Walichafua tu, hivyo tu. Wasingeweza kufanya hivyo.

Maana, Mungu alikuwa amemchagua mtu kwa ajili ya wakati huo, na akauchagua Ujumbe, na hata tabia ya mtu huyo na yale ambayo yangepita katika wakati huo, yale Yeye angeweza kuweka, jinsi ambavyo angeweza, kwa tabia ya mtu huyo fulani, Angeweza kuyapofusha macho ya wengine. Maneno ambayo mtu huyo angesema, namna alivyotenda, yangewapofusha wengine, na kuyafungua macho ya wengine. Mnaona? Yeye alimvalisha huyo mtu kwa namna ya mavazi aliyokuwa; tabia, shauku, na kila kitu jinsi tu ilivyompasa kuwa, alichaguliwa tu kikamilifu kwa ajili ya hao watu fulani ambao angewaita kwa ajili ya huo wakati fulani.

Wakati, wengine wangesimama na kumwangalia, waseme, "Vema, siwezi. Kuna … Si—siwezi kuona." Walikuwa wamepofushwa.

82 Yesu alikuja vivyo hivyo, amevaa, Mungu asiyepatikana na mauti amevaa mwili wa kibinadamu. Na kwa sababu Yeye alizaliwa katika hori, katika hori lililojaa samadi, si mahali pa kulaza kichwa Chake; alizaliwa, kwa kufikiri, akiwa amebandikwa jina haramu. Mnaona? Mambo haya yote aliyokuwa, na jinsi alivyokuja, mwana wa seremala, jinsi ambavyo hakuwa na elimu.

Kwa kiasi fulani, ulimwenguni, hekima ya ulimwengu huu, Yeye hakuwa na uhusiano wowote nayo. Hakuna hata moja ya ustaarabu wa ulimwengu huu, elimu, wala chochote kile, Yeye hakuwa na uhusiano wowote na jambo hilo. Kwa nini? Yeye ni Mungu. Ingepingana. Kama alijaribu kwenda kwenye seminari mahali fulani na kujifunza jambo fulani ambalo makanisa haya ya ulimwengu yalikuwa yakifanya, yale katika … Mbona, hata isinge- … mbona, hata isinge- … haingefanana kabisa na ufahamu Wake, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mungu.

Kwa hiyo, elimu, kusoma, seminari, na kadhalika, ni kinyume kabisa na mapenzi ya Mungu. Mfumo wote wa elimu ni kinyume cha Mungu. Kila kitu kinafundisha mbali na Mungu, wakati wote. Ninapomsikia mtu akisema ya kwamba yeye ni Dk, Ph.D., L.L.Q., hilo linamfanya kuwa mbali sana na Mungu, kwangu mimi. Mnaona? Yeye alijielimisha tu kiasi hicho mbali sana na kile alichoitiwa kweli kufanya. Hiyo ni kweli.

Angalia jinsi ambavyo sasa waliongozwa na Roho Mtakatifu.

83 Sasa, hilo halimaanishi ya kwamba watu wenye elimu hawaingii. Mwangalie Paulo. Mwangalie Paulo. Nafikiri hakukuweko na jamaa katika siku zake mwenye akili nyingi zaidi ya Paulo, ambaye alikuwa Sauli wa Tarso. Alielimishwa chini ya Gamalieli, mmoja wa waalimu mashuhuri sana wa siku hizo; Mwebrania mkuu, mwenye msimamo mkali, Mfarisayo wa madhehebu. Naye Paulo alilelewa chini yake. Yeye alijua dini yote ya Kiyahudi. Lakini wakati alipokuja kanisani, alisema, "Sikuja kwako kamwe katika elimu ya mwanadamu, na kadhalika. Kwa sababu, kama ungefanya hivyo, basi ungeliamini hilo. Lakini nilikuja kwenu katika nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu, ili imani yenu iwe katika Mungu." Haya basi. Mnaona? Hiyo ni kweli.

84 Wengi walijaribu kuwaiga watu hawa, bali walilivuruga jambo hilo kama tu wanavyofanya siku hizi. Kulikuwako na mmoja aliyeinuka kabla ya wakati wa Yesu, aliyeongoza watu mia nne. Nanyi mnajua jinsi Maandiko yalivyosoma juu ya mambo haya, yakijaribu kuyafanya jambo hilo kabla ya wakati wake. Na wengine wao walijaribu kumwigiza Yeye, nao walikuwa yote *haya*, *yale*, ama *yale* mengine. Naye alisema, "Katika siku za mwisho, namna watakavyoinuka Makristo wa uongo, katika siku za mwisho, na manabii wa uongo, na kuonyesha ishara na maajabu." Tuna hayo yote. Mnaona? Lakini hiyo haiondoi yaliyo halisi. Inalifanya tu liangaze vizuri zaidi, kwa sababu tuna Kristo halisi, si wa uongo.

85 Sasa, sasa, tunatambua basi ya kwamba Mungu aliwatuma manabii Wake. Hiyo ndiyo njia aliyokuwa nayo ya kuwaletea watu Neno Lake, kupitia midomo ya manabii Wake.

Basi angalia, mnajua, Musa alisema, kama unataka kusoma katika Kutoka sura ya 4, na aya ya 10 na ya 12. Musa alisema Mungu alinena naye. Mungu alinena na mwanadamu, mdomo kwa sikio. Naye akasema, "Mimi ni mzito wa kunena," Musa alisema. "Mimi, mimi sitoshi. Si—siwezi kwenda."

Yeye alisema, "Ni nani aliyemfanya mwanadamu kuzungumza, ama ni nani aliyemfanya bubu? Ni nani aliyemfanya aone, ama ni nani aliyemfanya asikie? Si mimi, Bwana?" Kasema, "Nitakuwa pamoja na kinywa chako." Mnaona? Kwa hiyo …

Naye Yeremia alisema, kama unataka kusoma hayo katika Yeremia 1:6. Yeremia alisema ya kwamba, "Mungu aliweka maneno kinywani mwangu." Mnaona? Yeye—Yeye alinena, kinywa kwa sikio, pamoja na nabii mmoja; kisha akanena kwa nabii huyo mwingine, hakuweza kujizuia kabisa, na kunena kupitia kinywa chake.

86 Yeye ana njia za kulitangaza Neno Lake, mwajua. Naam, bwana. Kwa hiyo mnaona Biblia ni Neno la Mungu, si neno la mwanadamu.

Musa alisema, "Mungu alinena nami kwa Sauti, nami nikamsikia. Niliandika yale aliyosema."

Yeremia alisema, "Nisingeweza kuzungumza hata kidogo. Na, muda si muda, midomo yangu ilikuwa ikinena, na—na—nami nilikuwa nikiandika." Mungu alinena kupitia midomo yake, na ikatimia.

Danieli, Isaya, na kadhalika, manabii hao wote walikuwa karibu tu sawa.

87 Mnajua, katika Agano la Kale pekee, ni zaidi ya mara elfu mbili wale manabii waliosema BWANA ASEMA HIVI. Sasa, kama mtu akisema BWANA ASEMA HIVI, si yule mtu anayezungumza. Kama angefanya hivyo, asingekuwa nabii, angekuwa mnafiki, mnaona, maana isingeweza (kamwe) kutimia; nafasi moja kati ya mara elfu kumi, mnaona, huenda wakakisia jambo hilo. Lakini kama ni BWANA ASEMA HIVI, Bwana Mungu amesema jambo hilo.

Kama ningesema, "Orman Neville asema hivi"; ndugu yangu aseme, "Bw. Mann asema hivi"; ningesema, "Ndugu Vayle asema hivi," huku, ama baadhi ya hawa ndugu wengine, ye yote wenu; ninanena uliyosema. Kama mimi ni mwaminifu, ninasema vile tu wewe ulivyosema. Kama mimi ni mwaminifu, ninasema tu yale uliyosema.

Na watu hawa, wakiwa ni manabii, walisema, "Si mimi. Sina uhusiano wowote nayo, bali ni BWANA ASEMA HIVI." Kwa hiyo Biblia ni BWANA ASEMA HIVI kwa manabii.

88 Angalia, walichukua Roho ya Kristo juu yao wenyewe, na kutabiri matukio ambayo yangetimia. Nena kuhusu utabiri! Walisema yale yangetukia kote katika nyakati, walipoketi, kusimama, kuweka, kutembea pamoja na Roho wa Kristo juu yao, hata wakatenda kama Kristo. Nao wasomaji wangesoma na kufikiri ya kwamba manabii walikuwa wakinena juu yao wenyewe.

Mnamkumbuka yule towashi alipokuwa anasoma Isaya 53:1, jinsi ambavyo, ya kwamba, "Alikuwa amejeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, kwa kupigwa Kwake sisi tumepona"? Yule towashi akamwambia Filipo, "Nabii huyu anamnena nani, yeye mwenyewe ama mtu mwingine?" Mnaona, nabii alinena kana kwamba ni yeye mwenyewe.

89 Mwangalie Daudi akilia katika Roho, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Mifupa yangu, wao wananikodolea macho mimi, mimi," Daudi. "Waliichoma miguu yangu na mikono yangu," Daudi. "Waliichoma miguu yangu na mikono yangu. Bali Wewe hutaiacha nafsi yangu katika kuzimu, wala hutamwacha mtakatifu Wako aone uharibifu," kana kwamba Daudi alikuwa akinena juu yake mwenyewe kuwa mtakatifu. Ilikuwa ni Mwana wa Daudi, ile Mbegu iliyozaa, ya kiroho ikishuka kupitia pale. Ingawa Daudi mwenyewe alikuwa gugu, lakini ndani yake kulikuwa na punje ya Ngano. Mnalipata?

Kwa hiyo, Biblia nzima si neno la mwanadamu, wala haikuandikwa na mwanadamu, kuletwa na mwanadamu, wala haiwezi ku—kufunuliwa na mwanadamu. Ni Neno la Mungu lililofunuliwa na Mungu Mwenyewe, Mfasiri Wake Mwenyewe, Kristo akijifunua Mwenyewe katika Neno Lake Mwenyewe.

90 Mwangalie Kristo amesimama hapa nyuma katika Daudi. Daudi hata hakuweza kufikiri sasa. Akili zake zilikuwa zimemtoka, tuseme. Naye alikuwa amening'inia msalabani, kama mnavyoona sanamu hii hapa; akining'inia msalabani, akilia, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha? Mifupa Yangu yote, wananikodolea macho. Waliichoma mikono Yangu na miguu Yangu. Walinichoma ubavuni." Mnaona? "Mbona uko mbali sana na Mimi? Mafahali wote wa Bashani wamenizunguka. Wanatikisa vichwa vyao, wakisema, 'Yeye alimtumaini Mungu, ya kwamba angemwokoa; sasa hebu tuone kama Yeye atamkomboa,'" akinena maneno yale yale.

Kwa hiyo, unaona, wakati Mungu alipodhihirishwa duniani hapa, Yeye alisema maneno yale yale Daudi aliyosema. Mnalipata? Kwa hiyo, unaona, si neno la mwanadamu; Ni Neno la Mungu. Kulikuwa na Mungu katika Daudi; huyo hakuwa Daudi. Yeye hakujua alilokuwa anasema; yeye alikuwa tu hivyo katika Roho.

Hivyo ndivyo Musa alivyokuwa. Yeye alikuwa hivyo sana katika Roho, alipitishwa katika kiwango alichokuwa akiishi, na akasimama pale uso kwa uso, katika kile kijiti kilichowaka moto, akizungumza na—na—na Mungu Mwenyewe. Kasema, "Vua viatu vyako. Ardhi unayosimama ni ardhi takatifu."

Ninawazia wakati Musa alipoondoka pale, aliwazia, "Ni kitu gani kilichotukia? Ni kitu gani kilichotukia? Ilikuwa ni kitu gani?

"Kasema,"Shuka uende Misri. Nitaenda pamoja nanyi."

Akasema, "Ni halisi kwangu, sina budi kwenda." Alimchukua mke wake na watoto wake … na—na mtoto wake, hasa, na fimbo yake mkononi mwake, kisha akashuka akaenda Misri, kuwakomboa watu. Mnaona?

91 Mungu akinena, Mwenyewe, kupitia kwa manabii. Mnaona, wao, wao … Si manabii; ilikuwa ni Mungu. Maana, nabii, wao wenyewe, wasingeweza kusema mambo hayo. "Ni nani aliyeamini habari zetu?" Isaya akisema, mnaona.

"Ni nani amesadiki habari tuliyoileta? Mkono wa Bwana amefunuliwa nani? Yeye atakua mbele yetu kama ndama katika—katika zizi. Na jinsi ambavyo, hata hivyo, alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Tuliponywa, kule nyuma mbali katika wakati huu hapa; na Isaya, huko nyuma miaka mia nane kabla ya Kristo. Mnaona? "Kwa mapigo Yake tuliponywa," wakati uliopita, tayari, "tumeponywa." Loo, jamani!

Jinsi, Neno la Mungu, lilivyo kamilifu sana! Liaminini, enyi watu. Ndicho kitu pekee kinachoweza kukuokoa.

92 Maneno mengine yote, sijali yamewekwa vizuri namna gani, namna gani, yanatoka wapi, yanatoka katika madhehebu gani, ama mtu huyo ni mwerevu namna gani, yanapaswa kupuuzwa kabisa, chochote kinyume cha Neno. Mnataka kuandika Andiko hilo, ni Wagalatia 1:8. Mnaona? Paulo alisema, "Ingawa sisi, ama Malaika kutoka Mbinguni, angehubiri jambo lingine lo lote isipokuwa Hili ambalo tayari mmesikia, na alaaniwe."

Kwa maneno mengine, kama Malaika angekujia kutoka Mbinguni, Malaika anayeng'aa sana, naye angesimama; kijana, hilo lingekuwa chambo kwa siku hii, sivyo? Malaika anayeng'aa sana akaja pale na kusimama, na kusema mambo yalikuwa kinyume cha Neno; unasema, "Shetani, ondoka kwangu." Sawa. Kama yeye ni askofu, kama yeye ni … cho chote alicho, usimwamini kamwe kama yeye hasemi sawasawa kabisa na Biblia hiyo, Neno kwa Neno. Mwangalie, yeye atakuchukua kwa Biblia hiyo sasa. Atakuchukua hadi mahali fulani, kisha alining'inize papo hapo. Unapoona Biblia ikisema jambo moja, kisha analiepa hilo, mwangalie papo hapo.

Mnaona, hivyo ndivyo alivyomfanyia Hawa. Alishuka moja kwa moja na kusema kila kitu sawasawa kabisa. "Vema, Mungu alisema jambo *hili*."

"Hiyo ni kweli, Hawa. Amina. Tunaamini jambo hilo, pamoja."

"Vema, Mungu alisema jambo *hili*."

"Amina. Tunaamini jambo hilo, pamoja."

"Mungu alisema jambo *hili*."

"Tunaamini jambo hilo, hakika."

"Vema, lakini Mungu alisema tutakufa."

"Vema, sasa, unajua Yeye ni Mungu mwema." Yeye hakusema hangefanya hivyo, mnajua. "Lakini hakika …" Loo, mimi! Huyo hapo.

Na kama alikuwa mdanganyifu namna hiyo, na Biblia ilisema, "Katika siku za mwisho angewadanganya walio Wateule kama yamkini," tunapaswa kuwa wapi leo, enyi marafiki? Sasa, masomo haya madogo ya shule ya Jumapili, yanapaswa kupelekwa karibu sana, mwajua, mioyoni mwetu, kuona … Tunapaswa kusikiliza kwa makini sana na kuona jinsi jambo hilo linavyodanganya.

93 Angalia, hatuwezi, hatupaswi, kusikiliza neno la mtu mwingine yeyote. Hatujali ni werevu namna gani, tumeelimika vipi. Biblia, katika Mithali, inasema, "Hatuna budi kutupilia mbali hoja." Mnaona? Sasa, hapa katika milki hii ya pili …

Ulimwengu wa kwanza ni hisi zako za kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Hiyo ni katika mwili wako wa nje.

Kwenye mwili wa ndani, ambao ni roho, kuna hoja na mawazo, na kadhalika. Hatuna budi kutupilia

hayo yote chini. Siwezi kutoa hoja, kusema, "Sasa ngoja, kama Mungu ni Mungu mwema …" Nasi tunaambiwa mengi sana siku hizi ya kwamba Yeye ni mwema. "Kama Yeye ni Mungu mwema, basi kama nikiwa mwaminifu, ingawa siwezi kuona jambo hilo katika Biblia kuwa ni kweli, ingawa mimi ni mwaminifu, nitaokolewa." Utapotea. [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

"Kama nikienda kanisani na kufanya tu mambo ninayoamini kwamba ni kweli, na kujaribu kushikilia yale ninayofikiri ni kweli, vema, mimi …" Ungali umepotea.

"Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, bali mwisho wake ni njia za mauti." Mnaona? Hutaokoka; utapotea. Mnaona? Mnaona? Haina budi kuwa ni Mtu yule wa ndani anayeongoza.

94 "Vema, nimenena kwa lugha, Ndugu Branham. Vema, hivi huamini katika kunena kwa lugha, Ndugu Branham?" Kabisa. "Vema, nilipaza sauti; huamini hilo?" Naam, bwana. "Ninaishi maisha mazuri ya Kikristo. Hivi hamwamini hayo?" Naam, bwana. Lakini bado hilo halimaanishi umeokoka. Wewe ni mtu mzuri; msafi, mwadilifu, mtakatifu, mtu mzuri.

Ndivyo walivyokuwa hao makuhani, wa dini kupindukia, wa dini sana mpaka kitu kimoja kikifasiriwa vibaya tu, wengepigwa kwa mawe wakafa. Hukumu ya kifo ya kulichezea Neno la Mungu ilikuwa ni mauti.

95 Hiyo ndiyo shida ya nchi yetu leo. Sababu ya sisi kuwa na mambo mengi sana yaliyolegalega duniani leo, adhabu si kali vya kutosha. Kama mwanamume akishikwa akitembea na mke wa mtu mwingine, wote wawili wanapaswa kuchukuliwa mbele ya hadhara ya umma na kuhasiwa, kweli, hadharani, kisha waachiliwe. Hiyo ni kweli. Kama mtu akishikwa akifanya jambo lo lote, akishuka kwenda barabarani, akiendesha kasi, haimpasi kupewa kifungo cha chini ya miaka kumi; yeye ana… anataka kuua makusudi. Mnaona? Ukiweka adhabu kama hizo juu yake, utawapunguza.

Lakini wakati wanasiasa wapotovu wanapoweza kupitisha *hili* hapa kwa hila, na kusema, "Vema, alikuwa anakunywa kidogo, alikuwa…hakukusudia kufanya jambo hilo." Naye angeua mtu mume, mtu mke, na kundi zima la watoto wasio na hatia, wamwache huyo Ricky aepuke, hizo ni siasa. Huo ndio ulimwengu. Huyo ni Ibilisi.

96 Mungu alisema kama mwanamume akishikwa katika uzinzi, ama mwanamke, watoe huko nje na uwapige mawe hata wafe. Hilo lilitosha. Mnaona? Kama hata ameshikwa akiokota uzito wa fimbo, siku ya sabato, "Mchukueni mkampige mawe." Waliishi kwa jambo hilo wakati huo. Na sasa, mnaona, hatuna sheria za namna hiyo leo.

Lakini Mkristo, kanisa, kile ninachozungumzia asubuhi ya leo, hiyo sheria ya Mungu iko moyoni mwako. Mnaona? Huna hamu ya kufanya jambo hilo. Iko ndani hapa. Unataka kuishika sheria ya Mungu kikamilifu sana. Haidhuru ni nini, unataka kuwa kile tu … Kama—kama Mungu anahitaji zulia la mlangoni, anakutaka uwe hilo zulia la mlangoni, unafurahi sana kuwa hivyo. Haidhuru ingekuwaje, unataka kuwa mlangoni. Mnaona? Chochote Mungu anakutaka ufanye, hicho ndicho unachotaka kufanya, maana ni Mungu. Sasa, hapo ndipo ambapo kweli unapata upendo wako halisi, wa kweli, wa kweli kwa Mungu.

97 Sasa tunaona basi, ya kwamba, "Malaika angehubiri jambo lingine lo lote," mbali na yale yaliyokwisha, ambayo tayari yamesemwa katika Biblia, "na alaaniwe." Hakuna mtu anayeweza. Siwezi kufanya hivyo; Haina budi kuwa namna hasa Linavyosema.

Na tena tunasoma, katika Ufunuo 22:18 na 19, "Kama mtu yeyote ataongeza neno moja kwenye Hili, ama kuondoa Neno moja Kwake, Mungu ataondoa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima." Sawa. Mungu atachukua sehemu yake, ingawa yeye ni mhudumu, hata awe nini, na neno lake … jina lake limeandikwa katika Kitabu cha Uzima. Mungu alisema, "Nitalifuta tu," hiyo ni kweli, "kama akiongeza jambo moja Kwake, ama akiondoa Neno moja Kwake." Hivyo ndivyo Mungu amelifanya Neno Lake kuwa lisilokosea. Mnaona? Unaweza kuongeza kwenye kanisa, ama kutoa kutoka kwa kanisa. Usiongeze kwenye hilo Neno, wala usiondoe Kwake, maana Mungu ataondoa jina lako moja kwa moja kwenye Kitabu cha Uzima. Na, hiyo ni, umekwisha basi. Mnaona? Huwezi kuongeza Kwake, wala kuondoa Kwake. Ni nini hasa hasa …

98 Haihitaji mfasiri, kwa kuwa Biblia ilisema ya kwamba Mungu hujifasiria Mwenyewe Biblia. "Si ya kufasiriwa kibinafsi," Petro alisema. Vema.

Na Maandiko yote yametolewa na Mungu, yamewekewa utaratibu Kiungu, na kitu hicho chote ni ufunuo wa Yesu Kristo. Agano Jipya na la Kale; ambamo walitabiri juu ya Kuja kwake, na kile angefanya atakapofika hapa, na yale angefanya katika wakati huu ujao. Kwa hiyo hilo linamfanya yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaona?

Kama vile katika Waebrania pale, wakati Paulo alipoliandika. Yeye ni Mungu, "Yesu Kristo jana," wa Agano la Kale. Yeye ni "Yesu Kristo leo," aliyedhihirishwa katika mwili. "Naye ni Yesu Kristo milele," katika Roho, "kuja." Mnaona? Mnaona? "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

Naye daima anaishi kulifanya Neno Lake liishi namna lilivyosema lingefanya kwa wakati huo. Yeye yu

hai.

99 Alikuwa hai katika Agano la Kale, akidhihirishwa. Ninataka tu kuwaacha muone kitu kidogo hapa, kama mnaweza kuvumilia. Angalia, wakati Yesu alipodhihirishwa katika Agano la Kale, kama tunavyoamini.

Sasa, ninyi wahubiri huko nje, mnaweza kubishana nalo, fanyeni lo lote mnalotaka, bali ninazungumza kwa ninii yangu … yale ninayowazia. Mnaona?

Wakati Yesu alipodhihirishwa katika Agano la Kale, katika mwili wa kiungu, katika utu wa Melkizedeki; si ukuhani, bali ni Mtu, Mtu. Mnaona? Kwa kuwa, Mtu huyu alikuwa bado hajazaliwa, bali alikuwa katika mwili wa kiungu, kwa hiyo hakuwa na baba, hana mama. Yeye alikuwa Mungu Mwenyewe. Yeye alidhihirishwa katika mfano wa Mwanadamu, aliyeitwa, "Mfalme wa Salemu, ambaye ni Mfalme wa Amani, na Mfalme wa Haki." Mnaona? Yeye alikuwa Melkizedeki. "Hakuwa na baba wala mama, mwanzo wa siku zake wala mwisho wa uhai wake." Mnaona? Ilikuwa ni Yesu katika mwili wa kiungu, katika umbo la Mwanadamu. Ungeweza kufanya jambo hilo? Vema.

100 Ndipo Yeye alifanyika mwili wa kibinadamu, na akakaa kwetu, katika Utu wa Yesu Kristo Mwenyewe, aliyezaliwa na bikira Mariamu. Yeye alikuja katika umbo hilo apate kufa, kisha akarudi Mbinguni.

Sasa katika siku hizi za mwisho, Yeye ameahidi kujidhihirisha Mwenyewe katika utimilifu tena, wa mwili Wake, katika Roho. Mnaona? "Kwa kuwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu." Sasa angalia Sodoma, namna ilivyokaa, na kile kilichotukia. Naye Yesu Kristo akidhihirishwa katika umbo la mwili, wa Kanisa Lake leo, mnaona, akifanya jambo lile lile, kazi ile ile, mambo yale yale aliyofanya wakati wote, hayabadiliki, Yule wa Milele. Mnaona? Na duniani leo, Yeye amejidhihirisha Mwenyewe katika miili ya wanadamu, miili yetu ya kibinadamu ambayo ameiita, na kufanya jambo lile lile hasa alilofanya katika nyakati nyingi, na katika nyakati za mwili Wake juu ya nchi. Na akifanya jambo lile lile leo, kwa sababu, "Mungu zamani alinena na baba zetu kupitia manabii, katika siku hizi za mwisho katika Mwanawe, Yesu Kristo." Mnaona, Mwana akifunuliwa katika siku za mwisho, Mungu akidhihirishwa katika mwili wa kibinadamu, ameketi kabla tu ya maangamizi ya Sodoma, mwisho wa ulimwengu wa Mataifa. Mnaona jambo hilo?

Kuna madhihirisho matatu.

101 Sasa, jambo lingine linalotukia, ni wakati yote yamekusanyika katika Mtu huyo mmoja, Yesu Kristo, Bibi-arusi na Mwili wa Bwana Arusi, kwenye kule kurudi katika mwili kwa Bwana Yesu. Kuzifanya mara tatu Kwake… Wakati alipoletwa duniani; aliuawa, akasulubishwa, akafufuka. Akijidhihirisha Mwenyewe katika umbo la Mwili Wake, ambao ni Bibi-arusi Wake, Mwanamke. Mnalipata? Yeye ni sehemu ya Mwili Wake.

Na mwanamke na mwanamume wako karibu sana, hata wao ni karibu tu … Wao ni wale wale. Wanapaswa kuwa, hata hivyo. Hao hapo, mnaona, walidhihirishwa vivyo hivyo kabisa. Yeye ni sehemu yake, kwa sababu aliondolewa kwake.

Na Bibi-arusi leo ametolewa kutoka katika mwili wa Kristo, ambao unatenda na kufanya vile vile hasa Yeye alivyosema ungefanya kwa siku hii, Bibi-arusi, Malkia; Mfalme na Malkia. Vema.

Tunachelewa sasa, kwa hiyo itatubidi kuharakisha na kumaliza.

102 Vema, Biblia nzima ni ufunuo wote wa Yesu Kristo, akijitambulisha kwa kila wakati. Yeye alijijulisha Mwenyewe katika siku za Luther, kama msingi; kanisa, unyayo, miguu.

Kama alivyofanya Mfalme Nebkadreza; mnakumbuka jinsi alivyoota ndoto hizo, na kutoka kichwani kwenda chini? Mnaona? Sasa Yeye anakuja tokea kwenye miguu kwenda juu. Mnaona? Katika ufalme wa Babeli alionyesha hayo yote ya Agano la Kale, alitoka kwenye kichwa akashuka chini, mpaka akashuka chini mpaka Mungu Mwenyewe akafanyika mwili chini ya miguu ya ngazi. Sasa hapa katika Agano Jipya, Yeye hujirudisha moja kwa moja tena, Kichwani tena, Kichwa cha dhahabu, apate kuvikwa taji. Mnaona? Angalia. Mnalipata?

Mnaona, Mungu alikuwako hapo mwanzo, naye aliendelea kushuka, kupitia manabii, na kuendelea, hata Mungu Mwenyewe akafanyika mwanadamu kama sisi, akashuka moja kwa moja hata kwenye miguu ya ngazi, mtoto aliyezaliwa katika hori; akachukiwa, akakataliwa, akadharauliwa, na jina baya, na kila kitu alichokuwa Yeye. Ndipo akaanza kuinuka, mnaona, na kutoka miguuni akaanza kulijenga Kanisa, Bibi-arusi, akirudi, kurudi; na sasa akija kwenye lile Jiwe la Kuweka Juu, ambapo yote unaungana pamoja na kufanya ule Mwili mmoja mkuu wa Yesu Kristo uliogeuzwa.

103 Mungu hufunuliwa katika kila wakati kwa Neno Lake lililoahidiwa kwa wakati huo. Sasa hebu na tuangalie baadhi ya ahadi Zake ni za nini leo, wakati tunafunga sasa katika maneno haya ya mwisho.

Sasa Mungu anajifunua Mwenyewe katika wakati wa Nuru ya jioni. Hebu tuone sasa. Tunaona …

Nina fungu moja tu la Maandiko yaliyoandikwa hapa. Kama mnavyoweza kuona kwenye ukurasa huu, ni Maandiko mangapi yameandikwa pale. Lakini, tuna kama dakika kumi na tano tu kabla ya saa sita. Ninataka kutoka nje. Nami sijapwelewa na sauti, asubuhi ya leo, nikizungumza. Wakati mwingine hizi viyoyozi hapa hunifanya nimepwelewa sana na sauti.

Kwa hiyo kama Ndugu Neville hataninii … Huna kitu cho chote kwa ajili ya usiku wa leo? [Ndugu Neville anasema, "La." — Mh.] Vema, vema, nita- … Kama ni sawa, nina kitu fulani. Niliona pakiti ya sigara, hivi majuzi, imelala mwituni; nami nina Ujumbe kutoka kwenye pakiti hiyo ya sigara, kwa ajili ya usiku wa leo, Bwana akipenda. Mnaona?

Kwa hiyo, nina Maandiko haya hapa. Nami sitaki kuchukua muda wa ziada, ili mweze kurudi.

104 Pakiti ya sigara, kuzungumzia. Vema. Nilikuwa nikitembea mwituni, na pale palikuwepo na pakiti ya sigara, nami nikaendelea tu kusonga mbele. Nikawaza, "Vema, mtu fulani yuko mbele yangu."

Ndipo kitu Fulani kikasema, "Geuka na uchukue hicho."

Nikawaza, "Chukua pakiti ya sigara? Si mimi."

Kitu fulani kilisema, "Geuka na uchukue pakiti hiyo ya sigara."

Nami nikashuka nikaenda kule, kulikuwako na pakiti tupu ya kale, nami nikaona kitu fulani. Nitawaambia kuhusu jambo hilo, usiku wa leo, Bwana akipenda. Vema.

105 Sasa tutazungumza kuhusu Nuru za jioni, kwa muda mfupi tu. Biblia inabashiri ya kwamba kungekuja wakati, karibu sana na wakati wa mwisho, ambapo jua lingechomoza, na kungekuwa na Nuru ya jioni. Sote tunajua jambo hilo. Sivyo? Sisi, sisi tuna … Sisi ambao tunaujua Ujumbe wetu leo kutoka kwa Bwana Yesu, tunaamini ya kwamba kutakuwako na Nuru ya jioni. Na hii Nuru ya jioni …

Bila shaka, ile Nuru kuu itakuja wakati Yesu Mwenyewe atakapodhihirishwa hapa duniani, ama kule Mbinguni, akimchukua Bibi-arusi Wake, kisha ule Utawala wa Miaka Elfu utaanza.

106 Lakini tuna moja ya nyakati za kutisha sana kupitia, ambazo zimewahi kuwekwa mbele za wanadamu. Nami ninaingojea tu saa hiyo, basi wakati tunapoweza kupata…kila mtu anapoweza kupata nafasi wakati ambapo mmepata likizo kazini na kutumia siku chache, nasi tunaweza kupatayarisha mahali fulani ambapo ninaweza kuzungumza juu ya vile Vitasa na mambo yatakayotukia katika siku za mwisho; na kuyaweka majuma mawili matatu pamoja, na kuyaleta hayo pamoja, kama Mungu akinijalia kuishi kufanya jambo hilo kisha anivuvie kufanya hivyo, tuone jinsi vitu hivyo vitakavyoingizwa ndani, na hizo Ngurumo. Ndipo mtaona yale ambayo mtu huyo na watu hao wamekuwa wakiota, na mambo haya yote pale, yatatimia; mnaona, mtaona kitu ambacho hizo zilifunua, hiyo ngurumo kuu inayokuja kutoka—kutoka mbinguni. Sasa, bila shaka, kundi zima la ninyi nyote, mnajua ya kwamba mimi ninajua kile ambacho—kile ambacho hiyo inamaanisha, mnaona. Na, lakini hebu na tungojee mpaka wakati utakapofika, mnaona, iwe hivyo, mnaona, sasa, na itakuwa zaidi katika majira yake.

107 Sasa, kwa hiyo tutasoma baadhi ya haya—haya Maandiko hapa ndani. Sasa, katika wakati wa jioni Nuru zinakuja, sasa, tunaona ya kwamba haina budi kuwe na Nuru ile ile iliyokuweko asubuhi.

Maana, hakuna jua moja asubuhi na jua lingine alasiri. Ni jua lile lile. Jua lile lile lililoko alasiri liko asubuhi; liko vile vile asubuhi kama lilivyo alasiri.

Sasa, ilisema, "Siku yenyewe," siku kati ya wakati huo, "itakuwa kwa namna fulani, loo, kama siku ya huzuni, giza. Isingeweza kuitwa mchana wala usiku, katikati ya hiyo."

108 Mnaona, huko ni kuumbwa kwa ule Mwili, kutoka miguuni, ukija juu. Wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alikuwa ni Mwana, Nuru, ndipo akauawa. Kanisa likachukua mahali pake, kisha kufia imani halafu likapitia kwenye zile Nyakati za Giza, na likaanza kujenga kwenye ule msingi likiwa linapanda juu. Basi uwezo wa kuona unatoka wapi? Juu ya kichwa.

Ona lile ono; Nebukadreza? Kumwona akishuka, tangu mwanzo wa wakati wa Mataifa kabla ya Damu kumwagwa kwa ajili yao na kufanya upatanisho. Walikuwa waongofu walioletwa. Lakini angalia lilishuka moja kwa moja, moja kwa moja chini, moja kwa moja mpaka chini, katika mfano, mnaona, lilishuka chini.

Ndipo likaanza moja kwa moja kurudi, likirudi, Kanisa likarudi kutoka miguuni, likipanda juu. Sasa ni wakati wa kichwa—wakati wa kichwa. Sasa angalia ile Nuru.

109 Huwezi kuona kwa mikono yako, hata hivyo ni sehemu ya mwili. Huwezi kuona kwa masikio, hata hivyo yanaweza kusikia. Huwezi kuona kwa pua, hata hivyo inanusa. Huwezi—huwezi kuona kwa midomo, ingawa hunanena; mnaona, huo ulikuwa ni wakati wa Kipentekoste. Lakini sasa ni katika wakati wa macho, kuona. Mnaona? Sasa, hakuna hisi inayosogea juu ya jicho. Hiyo ni kweli?

Ifuatayo ni akili, ambayo ni Kristo Mwenyewe, Ambaye anautawala Mwili wote.

Hakuna kusogea, msogeo kuzidi hiyo. Mnaona? Kila kitu kingine kimesogea. Mnaona? Sogeza miguu yako, sogeza misuli yako miguuni mwako, sogeza kila kitu. Sogeza … Masikio yako yanaweza kusogea, pua yako, midomo yako, na kadhalika. Lakini baada ya macho yako, hakuna kitu kinachosogea.

Hiyo ndiyo sababu wanadai ya kwamba watu wanakuwa na upara upesi, ni kwa sababu, mnaona, hakuna mazoezi ya kuendeleza misuli katika—katika nywele, kichwani. Mnaona? Nayo haina mto kusudi zinyonye damu mle ndani. Damu haiwezi kupitia pale, mnaona, haiwezi kwenda juu na kuipatia damu. Bila shaka, m—mzizi wa nywele huishi kwa damu.

Na sasa tunaona ya kwamba sehemu hiyo, mnaona, hakuna kitu juu ya jicho.

110 Sasa hebu na tuone. "Itakuwa Nuru" (yapata siku ya katikati?) "Wakati wa jioni!" Nuru inatumwa kwa ajili gani? Kwa hiyo unaweza kuona mahali ulipo … namna ya kuzunguka. Hiyo ni kweli? Angalia mahali ulipo. "Itakuwa Nuru wakati wa jioni."

Sasa, tunachukua hilo sasa na kulilinganisha na Malaki 4. "Kwa maana, angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, naye atawageuza wa—watoto wawarudie baba zao, na baba wawarudie watoto wao," (hiyo si ni kweli?) " "Nisije nikaipiga dunia kwa laana."

Sasa hebu tumchukue Yohana ama … Luka Mtakatifu 17:30, na angalia yale Yesu aliyotabiri pale, akisema ya kwamba, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, itakuwa vile vile …"

Sasa kumbuka, angalia, huu ni wakati ambapo Mwana wa Adamu angefunuliwa; kufunuliwa kwa Mwana wa Adamu. Sasa, Mwana wa Adamu kweli alifunuliwa kwa hali isiyo dhahiri, kwa muda mchache pale, kabla tu ya Sodoma kuteketezwa. Sasa, Mtu huyo alikuwa ni Elohimu. Huyo alikuwa ni Mungu; na Yesu ni Mungu. Basi Mungu alifunuliwa papo hapo kwa hali isiyo dhahiri kwa muda mchache, apate kuzungumza na Ibrahimu, katika ile hukumu ya upelelezi. Kwa muda kidogo tu, Mwana wa Adamu alifunuliwa; Mwana wa Adamu, Elohimu. Mnaona jambo hilo, enyi kanisa? [Kusanyiko linasema, "Amina." —Mh.] Mwana wa Adamu, Elohimu, alifunuliwa kwa dakika chache tu. Kwa kuwa, kesho yake asubuhi uliteketezwa, (lini?) Kabla jua halijachomoza tena.

Kwa hiyo hakuwezi kuwa na madhehebu yoyote yaliyosalia, wala hapawezi kuwa na maendeleo zaidi ya yale yanayoendelea sasa hivi, kwa kuwa utateketea kabla ya mapambazuko tena. Uamsho umekwisha, kote nchini. Hakutakuwako na ufufuo tena, miamsho mikubwa inayofagia; taifa hili kamwe haliupokei. Huenda ukawa na mkutano wa kielimu. Lakini, ninamaanisha, ufufuo wa Kiroho, tumeuona wote. Natumaini mnalipata. Ninayasema kwa njia ambayo—ambayo ninatumaini mtalipata. Mnaona? Imekwisha.

Mhudumu mzuri alisema, muda mfupi uliopita, alisema, "Ndugu Branham, laiti ningaliweza tu kuwa na furaha ya Bwana moyoni mwangu!"

Nikasema, "Mwanangu, ufufuo umekwisha." Mnaona?

111 Sasa viimarishi vimewekwa kwenye meli. Mawimbi makubwa ya kutisha yako hapa mbele zetu; bali tunajua, ng'ambo ya mawimbi hayo huko ng'ambo, tunakaribia ufukoni. Mnaona? Tunakaribia ufukoni. Kaeni tu imara. Kaeni tu katika Neno. Kaa na Mungu. Haidhuru unajisikiaje, ni kitu gani kingine chochote; dumu moja kwa moja na Neno. Hebu—hebu—hebu likae imara, wakati mnapoona mawingu haya yote makubwa ya kale yakituzunguka, na dhoruba zikija, na mabomu ya atomiki, na kila kitu kingine wanachozungumzia. Lakini kiimarishaji chetu kiko moja kwa moja katika Neno. Mungu alisema kingekuwepo hapa; tutapanda juu ya kila moja ya hayo. Naam, tutapita moja kwa moja juu ya hayo. Naam, kweli! Hivyo, hivyo haviwezi kutuzamisha Haviwezi kututosa majini. Utuweke kaburini; tutafufuka tena. Hivyo tu ndivyo ilivyo. Hakuna njia yo yote ulimwenguni ya kuizuia kule chini. Tutapanda kila moja ya hayo, maana Jemadari wetu Mkuu anatuita huko ng'ambo ya pili.

Tumetiwa nanga katika Yesu, tufani za maisha nitazistahimili;
Nimetia nanga katika Yesu, siogopi upepo wala wimbi;

112 Chochote kile, na kije. Cho chote kile, yo yote yatakayotukia, hayajalishi. Tumetiwa nanga papo hapo katika Yesu. Kama nikiishi, nitaishi kwa utukufu wa Mungu. Kama nikifa, basi ningeweza kufa kwa utukufu wa Mungu. Ni—ni—ninataka tu kuninii … Ni kwa utukufu wa Mungu, ndilo ninalotaka kufanya. Wakati hayo yote yamekwisha, sitaki kukaa tena. Ninataka kwenda ambapo … kwenye thawabu yangu aliyoninunulia mimi; si kile nilichopata, bali kile alichonunua kwa ajili yangu, kile alichonipa kwa neema Yake.

113 Kwa hiyo tunaona Nuru ya jioni iko hapa. Na ya nini kupata Nuru, kama huna macho yo yote ya kuona namna ya kwenda kila mahali katika Hiyo. Nuru ya jioni ni nini? Nuru inakuja, kufunua jambo fulani. Hiyo ni kweli? Kama kuna kitu fulani hapa, unajisikia na huwezi kuelewa ni kitu gani, gizani, basi washa taa. Ni kufunua! Malaki 4 itafanya nini? Mnaona? Fanya jambo lile lile. Kule kufunguliwa kwa zile Muhuri Saba kulikuwa kufanye nini, ambapo madhehebu haya yote yanayumbayumba kila mahali katika nini hii…? … Ni kufunua, kuleta nje. Kama huna macho yoyote, basi kuna faida gani kufunua? Hapana budi kuwe na

macho, kwanza, kuona. Hiyo ni kweli? Kufunua Malaki 4, kufunua Luka Mtakatifu 17:30, Yohana Mtakatifu 14:12, pia Yohana 15:24, 16:13. Na pia kufunua Ufunuo 10:1 hadi 7, kufunguliwa kwa ile Mihuri Saba, na Ujumbe wa malaika wa saba; kufungua, kufunua, wakati Nuru ya jioni inapokuja. Sasa kama mtu …

114 Katika Wakati wa Laodikia, watu walikuwa (nini?) "Uchi." Wao ni uchi? "Vipofu." Nuru inamfaa nini kipofu? Kama kipofu akimwongoza kipofu, si wote wataanguka shimoni? "Uchi, kipofu, wala hujui." Hata akili zao zimekwisha, uwezo wao wa kiroho wa akili, ufahamu wa kiroho. Mnaona?

"Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wasiopenda walio wema; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake." Nguvu za ufunuo; hata hawauamini. Mnaona? Hawaamini katika vitu kama manabii. Na kwa hiyo hawaliamini. Wao wanaamini ya kwamba—ya kwamba Malaki 4 ni kuwa kanisa fulani ama madhehebu fulani.

Alipokuja mara ya kwanza, alikuwa mwanadamu. Alipokuja mara ya pili, akiwa na sehemu maradufu, alikuwa mwanadamu. Wakati alipokuja katika mfano wa Yohana Mbatizaji, alikuwa mwanadamu. Mnaona?

Katika siku za mwisho, wakati Nuru za jioni zitakapoanza kung'aa, macho yatafunguka na utaona unakoelekea. Ndipo ule Mwili tayari umeumbwa, ukisimama kwa miguu yake, ukisonga mbele, ukisonga mbele kwa Roho Mtakatifu. Nini? Yeye yule aliyewaendea manabii walioiandika Biblia, Roho Mtakatifu yeye yule akitenda kazi katika Mwili uliojazwa na Roho Mtakatifu, alitenda kazi katika Roho Mtakatifu, kutoka katika kila dhehebu, kila jamaa, lugha, na watu.

115 Bibi mdogo hapa, yeye si mfuasi wa madhehebu haya, ama madhehebu haya … ni mfuasi wa kusanyiko hili. Yeye anatoka mahali pengine, naye akaja asubuhi ya leo, akachukua picha pale. Alikuwa … akampa mwanangu, ambaye alishangaa sana. Sijui kama aliwahi kusikia jambo Hili ama la. Sijui. Alikuwa na picha ya Malaika huyu wa Bwana ambaye alikuwa kwenye zile Nyakati Saba za Kanisa, zile Muhuri Saba zilifunguliwa, kule nje, wakati ilipotukia. Kasema, akaangalia huko nyuma, naye akaona jambo hilo limesimama angani, katika ndoto. Naye akaangalia huko nyuma na kuona jambo hilo, akamwona mtu aliyevaa nguo nyeupe, akienda mbele; na nyuma yake, kasema inaonekana … Kasema, "Ndugu Branham, ilikuwa ni wewe." Kisha kasema, "Ukasonga mbele kuingia pale," kasema, "nyuma yako, walikuweko watu wa rangi mbalimbali, wamebeba bendera; Georgia, Alabama, mikoa mbalimbali, wakisonga mbele kwa hatua taratibu," wakipanda kuja kwenye kichwa ambako Kristo alikuwa akifunuliwa katika lile ono. Loo, haleluya!

116 Tuko katika siku za mwisho, na saa za mwisho za siku hizi. Unamwona sasa katika Neno Lake, na Neno Lake lote likidhihirishwa papa hapa mbele zetu? Loo, Kanisa la Mungu aliye hai, simama kwa miguu yako, mwamini Yeye kwa yote yaliyo ndani yako. Shikilia hilo Gurudumu dogo katikati ya gurudumu, liache liimarishe kila mwendo na kila mwendo utakaofanya. Kila wazo ulilo nalo, jalia litawaliwe na Mnara huu ulio ndani yako. Kwa sababu, Mungu ameketi moja kwa moja katika Neno Lake la wakati huu, katika Nuru ya jioni, akionyesha Nuru.

117 Upofu wa popo! Ungeweza kuwasha taa, na popo angekuwa kipofu sana asingeweza kuruka. Bundi aliaye, hao hayawani wote wa usiku, na vitu kama hivyo, mende na kadhalika, hawawezi kuona mchana. Hawajui yote yanahusu nini. Hawawezi kuona.

Na Nuru za jioni zimekuja. Kila mfano, kila mahali tuendapo, kwenye maumbile, kwenye Biblia, kwenye ka— kanuni ambazo Melk-…ambazo Danieli aliona, na—na mfalme wa siku hizo, wote waliona; na mambo haya yote, kila mtu, kila hali, kila mwendo, kila mahali katika ule Mwili, vinatuonyesha mahali gani hasa kwenye saa tunayoishi. Hakuna hoja nyingine inayoweza kuja juu yake.

Kulikuwa na zamu ya mkono; upendo, Wesley. Kulikuwa na zamu, ya msingi; Luther. Upendo, hapajakuwepo na mkubwa zaidi kamwe; uliitwa uamsho wa Wesley. Waliwatuma wamishenari ulimwenguni kote. Mmoja wa miamsho mikubwa sana iliyopata kufanywa, katika wakati uliotangulia huo.

Ndipo ukaja wakati wa Pentekoste; kisha ikaja katika vidole mbalimbali na kadhalika, wakati wa Kipentekoste, wa lugha, na pua, na kadhalika.

Sasa uko kwenye macho. Utahitaji macho ya nini, ama kuhitaji Nuru, kama macho hayo hayakuweko hapo yapate kuona? Hapana budi kuwe na macho, kwanza, kuweza kuona. Kisha hayo yalipokuja, Yeye akazifungua zile Muhuri Saba na kuifunua Nuru ya jioni, akichukua siri zote zilizofichwa kote katika nyakati hizi za kanisa, na sasa akazifunua kama alivyoahidi kufanya katika Ufunuo 10:1 hadi 7. Tuko hapa leo tukiketi katikati ya Neno, na Neno likifunuliwa kwetu na Yesu Kristo. Halafu, *Hili* ni Neno la Mungu.

118 Na ili tuwe raia Wake, hatuna budi kutembea karibu na Mwandishi wake, kusudi tupate kulielewa, kusudi lipate kufunuliwa. "Ee Bwana, utanitaka kufanya nini? Kama inanibidi kwenda mashambani na kuihubiri Injili, ama yanibidi kukaa nyumbani? Haidhuru ni nini, kama sina budi kuwa mke mzuri wa nyumbani, kama lazima niwe mama mzuri, kama sina budi kufanya hili, lile, ama lingine? Chochote kile, kama yanipasa budi kuwa mkulima, kama mimi … Chochote kile, Bwana, ungetaka nifanye nini?"

Si hivyo ndivyo Sauli alivyopaza sauti kule chini, "Bwana, ungetaka nifanye nini?" Alikuwa huko chini kwenye ninii … akienda zake kwenye—kulifunga kanisa lote gerezani. Lakini basi alipaza sauti, "Ungetaka nifanye nini?" Wakati ile Nuru ilipowashwa, kama Nguzo kubwa ya Moto ikining'inia juu yake. "Ungetaka nifanye nini?"

Nafikiri hilo ni neno zuri la kufunga, na kusema, "Bwana, ungetaka nifanye nini? Ninapoona Maandiko haya yamefunuliwa kikamilifu hivi sasa; Bwana, ungetaka nifanye nini?"

Na tuinamishe vichwa vyetu.

119 Nataka kila mtu hapa kujichunguza mioyo yenu sasa na kuuliza swali hilo, "Bwana, ungetaka nifanye nini?" Nanyi watu, kama mngali mko kwenye simu huko nje kila mahali nchini, inamisheni vichwa vyenu na muulize, "Bwana, ungetaka nifanye nini? Tukiona ya kwamba tuko hapa katika hizi siku za mwisho na masaa ya mwisho, yakiwa kikamilifu sana mbele zetu, yamefunuliwa wazi mno, ungetaka nifanye nini?"

120 Mungu mpenzi, wakati wanakuuliza swali hilo; Ninaomba, mimi mwenyewe, Kwako, ungetaka nifanye nini, Bwana, kwa kuwa ninatambua ya kwamba kila siku haina budi kuhesabiwa. Nami ninaomba ya kwamba utanisaidia, Bwana, kuishi ili kwamba kila siku, itahesabiwa kwa heshima Yako na utukufu.

Ninaomba ya kwamba utamsaidia kila mtu kote nchini, na wale walio hapa maskanini tunapoichunguza mioyo yetu na kusema, "Bwana, ungetaka nifanye nini? Ningeweza kufanya nini, Bwana, kuuendeleza Ufalme Wako na Huduma Yako?" Tujalie, Mungu.

Tuchunguze, mioyo yetu, na utujaribu. Kama kuna uovu wo wote ndani yetu, Bwana, uchoyo wo wote, makusudi yo yote mabaya ama nia mbaya, Ee Mungu, tusafishe kwa Damu ya Mwanao, Yesu Kristo, ambaye kwa unyenyekevu tunaukubali upatanisho wa mauti Yake na kufufuka Kwake. Na tukiwa tumehesabiwa haki kwa kuamini ya kwamba Yeye alifanya jambo hili, kwa furaha tunakubali mpango wa wokovu ambao Wewe hutupa, kwetu.

Baba, tunakushukuru kwa ajili ya Ujumbe wa siku hii, yale tunayoamini na yale tunayoshikilia, kujua na kuamini ya kwamba ni Neno Lako na Ujumbe Wako. Si kuwa tofauti na watu wengine, bali kujaribu kuwa zaidi kama Yesu Kristo Ambaye ni mfano wetu.

121 Mungu mpendwa, hapa kuna leso, na kuna wagonjwa kila mahali. Nami mwenyewe, Bwana, nimechoka na kudhoofika, asubuhi ya leo. Ninaomba ya kwamba utatusaidia, Mungu mpendwa. Tunakutegemea Wewe ututie nguvu. Wewe ndiwe Nguvu zetu. Umewasaidia wengi sana, Mungu mpendwa.

Hivi majuzi, nikiwaza kule chini mwituni, nikitembea na Ndugu Banks Wood, wakati madaktari … Moyo wake ulikuwa mbaya sana hata ilikuwa vigumu kutembea. Halafu kufikiri namna mimi…sikuwa na fununu hata kidogo kule juu, nikitembea kwenye ile milima baada ya lile ono, "Sina budi kumpata huyo simba. Sina budi kuona simba huyo akiuawa."

Halafu nikishuka kuja kule, na nikisimama kule Tucson, kwenye Mkahawa wa Furr, na kuziona nguo zake zote zimening'inia chini, macho yake yemeingia ndani. Kasema, "Mungu, kama unaweza kuonyesha ono, alipo simba, hakika unaweza kuonyesha kumhusu Ndugu Woods."

Na ndipo ikaja, "Weka mikono yako juu yake."

Naye yuko hapa leo, amerudi, Ndugu yetu Banks tena, mwenye nguvu, akipanda huku na huko kwenye milima hiyo. Namna tunavyokushukuru Wewe, Mungu mpendwa. Wewe ni Mungu yule yule kwetu sisi sote kama ambavyo ungekuwa kwa Ndugu Woods. Ninajua unampenda, kwa sababu yeye ni mtumishi Wako, mwaminifu na mnyofu.

122 Nami ninaomba, Mungu mpendwa, ya kwamba utamshughulikia kila mmoja wetu, na utusamehe dhambi zetu, na kuponya magonjwa yetu ya miili yetu. Tufanye tufanane zaidi na Wewe, siku baada ya siku, Bwana, mpaka tutakapokuja katika kimo hicho kikamilifu cha Yesu Kristo. Tujalie, Bwana. Ninatumaini ya kwamba umechunguza kila moyo, sasa, nasi tunajua la kufanya. Tunakuomba utubariki sasa, katika Jina la Yesu.

123 Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu, kuna ye yote aliyeko hapa, ama kule nje kwenye—kwenye simu kila mahali nchini, ambaye angetaka tu, huku mkiomba, na vichwa vyenu vimeinamishwa, hebu umwinulie tu Mungu mkono wako sasa. Hivyo tu ndivyo unavyoweza kufanya; kuna msongamano humu asubuhi hii. Hivyo tu ndivyo unavyoweza kufanya; kuna msongamano humu asubuhi hii. Mwinulie tu Mungu mkono wako, useme, "Mungu, nifanye zaidi kama Yesu. Nataka kuwa zaidi kama Yesu." Mungu akubariki. Huko nje kila mahali nchini, mikono kila mahali, umati mkubwa mno. Pia, wangu umeinuliwa. "Ninataka kuwa kama Yeye zaidi. Nichunguze, Bwana, uone kama kuna uovu wowote ndani yangu; uondoae. Na—nataka …" Nini? Tuko hapa muda tu fulani, hata hivyo tutaondoka kama wewe una-…kama, haidhuru wewe u nani, u tajiri jinsi gani, u maskini jinsi gani, u kijana jinsi gani, u mzee jinsi gani.

124 Nilipokuwa nimesimama jana kati ya kundi do—dogo la watu maskini kule juu sana kwenye mlima fulani, kule chini kwenye…kwenye kijito. Kulikuwa na familia ndogo pale, mtu niliyekuwa nikizungumza naye juu ya Mungu, kwa muda mrefu sana. Akashuka akaja, maskini mkewe, watoto saba ama wanane; yeye, maskini jamaa mrefu aliyekonda, huko nje akijaribu kufanya kazi, dola chache kwa siku. Na mtu fulani akamruhusu kuishi katika kijumba kidogo. Na huyo pale mke wake juu pale, karibu tayari kupata mtoto mwingine, naye alikuwa na shoka kubwa na pana kule juu, akikata kuni, kuziangusha; mtoto mchanga kwenye paja moja, akizivuta zile kuni pamoja na mtu mwingine; akashuka akaja kukata kuni hizo, kuhifadhi maforsadi kwenye makopo, wasije wakapata njaa kwenye msimu wa kipupwe. Jamani, namna tulivyomsikitikia! Mimi na Ndugu Woods tulienda tukachukua gari, na tukaenda kule na kukata kuni zake, na kuziingiza ndani. Yeye, maskini mwanamke mwenye shukrani, amesimama tu pale. Nilimsikitikia. Nasi tuliendelea kuwaombea.

125 Na mtoto wake mchanga akapatwa na kifafa. Tulienda tukamwombea mtoto huyo mchanga, naye Mungu akamponya. Na hivi majuzi, mumewe alikuwa na ngiri, naye aliiingia ndani …

Nimekuwa nikizungumza naye. Alivuta sigara, wote wawili. Alitumia tumbaku, naye akafanya hivyo, pia, mfano wa watu wa milimani. Na ndipo nikaendelea kuzungumza nao juu ya jambo hilo. Na jana asubuhi nilipoenda kule, kwenye mapambazuko, huyu hapa yule mwanamume anakuja akitembea, ameunganisha mikono yake pamoja, na akasema, "Ndugu Billy, mimi ni mtu aliyebadilika." Akasema, "Nimevuta sigara yangu ya mwisho, nami niko upande wa Bwana."

Akasema, "Nilivuta tu sigara yangu ya mwisho, pia."

Loo, panda mbegu! "Mimi Bwana nimemwagilia maji. Nitaitia maji mchana na usiku, wasije wengine wakainyakua kutoka mikononi Mwangu."

126 Ee Mungu, turehemu sasa, ninaomba, na utupe shauku ya moyo wetu, maana mioyoni mwetu tunataka kukutumikia. Sasa, Baba, wote wako mikononi Mwako, kila mahali. Hao ni watoto Wako. Washughulikie kulingana na rehema, Bwana; si katika hukumu, bali katika rehema. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

127 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Moyo wako wote! Sasa, ninyi mlio na leso, mnaweza kuzipata.

Na sasa, ibada zetu, nafikiri zinaanza mapema kidogo, saa saba, ama kitu kama hicho. Ndugu Neville atalitangaza, katika dakika moja, kuhusu wakati wa kuanza.

Kuna ubatizo, nadhani, asubuhi ya leo? [Ndugu Neville anasema, "Maji yako tayari." — Mh.] Maji yako tayari, kama mtu fulani yuko hapa na bado hajabatizwa katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, mbona, hakika ni … Maji yako tayari kwa ajili ya ibada ya ubatizo.

128 Tunawathamini ndugu wote wahudumu. Ninamwona Ndugu … Mkutano wako ulikuwaje, ulienda sawa, Ndugu Parnell? Na Ndugu Martin, na, loo, wengi wao hapa, Ndugu Lee Vayle. Loo, kuna wahudumu tu kila mahali. Hakika tunathamini wewe kuwa hapa, ukishirikiana nasi katika Neno.

129 Labda huenda usikubaliane nami kabisa juu ya Hili; siwaombi mfanye hivyo, mwaona. Jambo pekee, hebu wazia tu jambo Hilo. Yale mnayoniambia, ninayawazia. Kama wahudumu wangechukua kanda hiyo, nao wanasema, "Vema, sikubaliani nayo." Hilo ni sawa, ndugu yangu. Huenda ikawa labda unawachunga kondoo fulani; wa—walishe cho chote unachotaka kuwalisha.

Ninajaribu sana niwezavyo kudumu kwa unyofu na Neno, kwa ajili ya hawa ambao wamewekwa mikononi mwangu kwa ajili ya Mungu, maana kondoo huhitaji chakula cha kondoo, bila shaka. "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu." Na hilo ndilo tunaloishi kwalo, kila Neno litokalo… Si wote … Si Neno tu mara kwa mara; bali kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu, hilo ndilo watakatifu wanapaswa kuishi kwalo.

Hebu na tusimame sasa kwa miguu yetu. Tunapoinamisha vichwa vyetu …

Na Ndugu Neville, una jambo fulani unalotaka kuwaambia? [Ndugu Neville anasema, "La." — Mh.] Ndugu Mann? Vema.

Kila mtu anajisikia vizuri? Sema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Vema.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu. Nitamwomba Ndugu Lee Vayle kama atakuja hapa, ama anaweza. Tafadhali nenda kule, Ndugu Vayle, kama ukiweza.

Ndugu Vayle ni ndugu yetu hapa, mwandishi wa vitabu hivyo. Naye anakiandaa kitabu sasa, Nyakati Saba za Kanisa, na akifanyia kazi na ile Muhuri Saba. Nasi hivi karibuni tutatarajia kuwa navyo hivi karibuni. Vema. Ndugu Lee Vayle.

Mungu akubariki.

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7